# Nipashe

Jumatano Aprili 21, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580557

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Mama** aomba msaada wa kukamatwa baba anayedaiwa kumlawiti mtoto

UKURASA 2



**Rais** auawa baada ya kuwatembelea wanajeshi vitani

UKURASA 19

**Klopp: Kiatu kinamfanya Salah kuwa mbinafsi**

UKURASA 21

# TRA yawaangukia wafanyabiashara

UKURASA 2






Baadhi ya maduka yakiwa yamefungwa katika mitaa ya Kariakoo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# Harmonize, Kajala na Paula wahojiwa kashfa mtandaoni



UKURASA 3

## NIDA yapata mwarobaini ucheleweshaji vitambulisho

UKURASA 2


**MICHEZO** VUNJABEI AIMWAGIA SIMBA BILIONI 2 UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Aomba msaada kukamatwa mumewe

**Na Yasmine Protace**

MKAZI wa Kivule Matembele, jijini Dar es Salaam, Shukurani Nestory, ameiomba serikali na asasi zisizo za kiserikali kusaidia kukamatwa kwa aliyekuwa mumewe, Abdul Idd Msangi, aliyetoroka na watoto wawili wadogo.

Akizungumza na Nipashe katika ofisi ya Kata ya Kivule, alidai mwanamume huyo alitoroka baada ya kufunguliwa shtaka la kumlawiti mtoto wake wa kiume mwenye umri wa miaka tisa ambaye ni mwanafunzi wa darasa la tatu katika shule mojawapo jijini Dar es Salaam.

Akisimulia mkasa huo alisema walibahatika kupata watoto wawili wa kiume baada ya kufunga ndoa mwaka 2012 na kutengana mwaka 2019 huku watoto wakibaki kwa baba yao.

"Katika ndoa niliishi kwa vipigo, manyanyaso na mateso, nimeteswa mpaka nilipoteza watoto wawili kwa kufia tumboni kutokana na vipigo, pia tulijaliwa watoto wawili wa kiume ambao mmoja ana miaka tisa na mwingine minne," alidai.

Kwa mujibu wa Shukurani, baada ya kutengana alijishughulisha na biashara ya kutembeza mboga na kupangisha chumba na alimuomba mzazi mwenzake ampatie watoto, lakini alikataa, baada ya muda alielezwa kuwa mwanawe anapitia mambo mabaya na kutakiwa kwenda shuleni.

Alisema alikwenda shuleni na mtoto alimweleza madhila anayoyapitia ikiwamo kulawitiwa na baada ya kukaguliwa ilibainika amefanyiwa ukatili huo.

Shukurani alisema alimpeleka mtoto kituo kidogo cha polisi Kitunda na kufungua kesi pamoja na kupewa PF3 yenye kumbukumbu 00-66-70, ambayo ilimwezesha kumpeleka mtoto kwenye matibabu na kugundulika kuwa ana vidonda katika sehemu ya haja kubwa kutokana na kutendewa vitendo vibaya.

Alisema kuwa wakati mzazi mwenzake akiwa mahabusu alikuja shemeji yake ambaye aliwachukua watoto kwa madai kuwa yule mmoja aliyefanyiwa ukatili anampeleka hospitali nyingine kwa uchunguzi zaidi.

Alisema aliondoka na watoto na ilipofika asubuhi shemeji yake alimwambia kuwa mzazi mwenzake katoroka na watoto usiku wa saa 10 kwa kutumia pikipiki. "Mtu alikuwa mahabusu aliwezaje kuachiwa na kuja kuchukua watoto kisha akatoroka nao," alihoji.

Askari katika Dawati la Jinsia kituo cha Polisi Stakishari, Fulgence Byangwamu, alisema matukio ya ukatili ni mengi hasa kwa wanafunzi na yanaripotiwa.

Aidha, alisema upelelezi unaendelea wa tukio hilo ili mtuhumiwa akikamatwa afikishwe mahakamani.

Mwalimu wa darasa la tatu katika shule hiyo, Boniface Mng'ong'o, alisema mahudhurio na afya ya mtoto huyo hayakuwa ya kuridhisha pamoja na kuimuita baba yake kumweleza, lakini hakutoa ushirikiano.

Mratibu wa Elimu Kata ya Kivule, Urumbi Kitila, alisema mifarakano ya wazazi ni chanzo cha matukio ya ulawiti na baadhi ya familia kulala chumba kimoja na watoto, hali inayochangia watoto kujifunza kupitia wazazi.

Alisema sababu nyingine ndugu kulazwa na watoto wa kiume kunachangia matukio ya ulawiti na kubaka, na kwamba licha ya elimu kutolewa haijasaidia kutokana na watoto kutotoa taarifa wanapofanyiwa ukatili huo.

Alisema shuleni kuna watoto wanaotendewa matendo hayo na wanapoona hawakai vizuri darasani na kuhojiwa atasema kalawitiwa na baba au mjomba.

Ofisa Maendeleo wa Jamii Kitunda, Anna Masawe, alisema kuwa utovu wa nidhamu ndio sababu kubwa ya matukio ya ukatili.

Alisema jamii ingekuwa inatoa ushirikiano matukio hayo yangepungua, lakini kwa sasa kesi nyingi zinamalizwa nyumbani.

# TRA yawaangukia wafanyabiashara

MAMLAKA ya Mapato (TRA), imeanza kampeni ya mlango kwa mlango ambayo imesaidia kuongeza mapato mwamko wa ulipaji na kurekebisha kasoro zinazojitokeza wakati wa ulipaji kodi kwa hiari bila kushurutishwa.

TRA imesema kumekuwa na mwamko mkubwa wa wafanyabiashara kulipa kodi kulinganisha na awali, walipowaona maofisa wa mamlaka hiyo, waliwakwepa na hata kufunga maduka.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipa Kodi kutoka TRA, Richard Kayombo, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kampeni ya elimu ya mlango kwa mlango inayoendelea katika mikoa mbalimbali nchini.

"Mwamko wa ulipaji kodi umeongezeka wafanyabiashara wamekuwa wepesi kwa sababu wameona tunafanya hivi kirafiki, wamekuwa wepesi kujieleza, hata hofu imeondoka, zamani walipotuona walikuwa wanafunga maduka.

"Sasa hivi wanatusikiliza na kutoa ushirikiano, elimu ya mlango kwa mlango imeleta mwamko mkubwa na baadhi ya mikoa tuliyofanya hili mameneja wamekiri idadi ya walipakodi wanaojisajili baada ya kuwatambua imeongezeka na wanaokadiriwa na kulipa malimbikizo wamejitokeza kwa wakati," alisema.

Alisema wamepokea malalamiko, maoni na matatizo ambayo ni sugu na kuyafanyia kazi.

Kayombo alisema malalamiko ya wateja wanayashughulikiwa ndani ya siku tano kwa mujibu wa mwongozo wa kumhudumia mteja na yale ambayo ni ya muda mrefu, nayo yanafanyiwa kazi.

Alitaja mikoa ambayo kampeni hiyo imefanyika kuwa ni Geita, Kinondoni, Arusha, Dodoma, Singida, Pwani, Mtwara na Mbeya, Mwanza huku akisisitiza kuwa wapo kwa ajili ya kuelimisha na siyo vinginevyo.

Alisema kwa sasa wapo mikoa ya Kilimanjaro, Ilala na Temeke na kusisitiza kuwa suala hilo ni endelevu ili kuhakikisha idadi ya walipakodi inaongezeka siku hadi siku.

Pia, Kayombo alisema elimu ya mlango kwa mlango imesaidia kurekebisha kasoro zinazojitokeza wakati wa ulipaji wa kodi kwa hiari bila kushurutishwa.

Alisema kiasi cha fedha walichokikusanya baada ya elimu ya mlango kwa mlango watakitangaza baada ya kumalizika mwaka wa fedha 2020/21.

Kadhalika aliwataka mameneja wa wilaya na mikoa wa TRA kufuata mwongozo huo ili kupunguza malalamiko na endapo mteja hajaridhika, ana uhuru wa kupelekea ngazi inayofuata.

"Tunaomba wafanyabiashara, maofisa wetu wanapopita kuelimisha kwa njia ya mlango kwa mlango, wawape ushirikiano kwa sababu lengo ni mlipakodi ahudumiwe mahali alipo." alisema.

Mkurugenzi huyo alisema waliamua kuwafikia wateja wao mlango kwa mlango baada ya malalamiko yanayohusu makadirikio na huduma na baadhi ya vitendo vya maadili kutoka kwa baadhi ya watumishi wa TRA.

Pia, alisema kumekuwa na uhitaji wa maofisa wa TRA kuona uhalisia wa biashara zao ili wanapokadiriwa kodi ziendane.

Alisema wanapowatembelea wateja, wanawashirikisha pia wakuu wa mikoa na wilaya na mamlaka za serikali za mitaa ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

Alisema elimu hiyo imesaidia kuwatambua waliosajiliwa na kupata Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) na ambao bado wanaongozwa ili wasajiliwe.

Kayombo alisema kampeni hiyo pia imewezesha kuwatambua waliokadiriwa kodi na kuzilipa na wale ambao bado wanawashawishi kufanya hivyo ili kuepuka adhabu.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akipata ufafanuzi wa jambo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa alipofanya ziara kwenye shirika hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# NIDA yapata mwarobaini wa vitambulisho

**Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imesema imeshashughulikia tatizo lililokuwa likichelewesha uzalishaji wa vitambulisho hivyo na kwamba ifikapo Julai, mwaka huu, watu wote waliosajiliwa watakuwa wamevipata.

Msemaji wa NIDA, Geofrey Tengeneza, alisema jana kuwa kutokana na kuwapo malalamiko kuhusu ucheleweshaji wa utoaji wa vitambulisho vya taifa, mamlaka imelifanyika kazi suala hilo.

Alisema mashine zilizokuwa zikitumika mwanzo zilikuwa na uwezo mdogo lakini kwa sasa wameshafunga zingine mpya zitakazomudu uzalishaji kwa haraka.

Mashine hizo mpya, alisema ziliagizwa kutoka Ujerumani na tayari zimeshaanza uzalishaji na zitakuwa zikitoa huduma kwa nchi zima, hivyo wananchi watembelee ofisi za mamlaka zilizo karibu yao kwa ajili ya kuchukua vitambulisho vyao huku vingine vikiendelea kuzalishwa.

"Ni kweli kwamba siku za nyuma kumekuwa na hilo tatizo la vitambulisho kuchelewa lakini kwa sasa tumeshakwisha pata mashine mpya ambazo uwezo wake ni mkubwa na tayari zimeanza kuzalisha toka Februari na kutawanywa. Kwa hiyo watu wote wenye malalamiko muda si mrefu vitambulisho vitawafikia," alisema Tengeneza.

Aliongeza kuwa mashine walizonazo mpya ni mbili na kila moja ina uwezo wa kuzalisha vitambulisho 4,500 kwa saa tofauti na zile za zamani ambazo zilikuwa zinazalisha vitambulisho 500 kwa saa.

Pia alisema mamlaka imeweka mikakati mbalimbali ili kushughulikia changamoto zote zinazoweza kujitokeza katika kukamilisha uzalishaji na usambazaji wa vitambulisho na hatimaye kuwafikia wananchi kwa wakati.

# Harmonize, Kajala na Paula wahojiwa kashfa mtandaoni

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limesema linachunguza tuhuma za kusambaa picha za utupu za msanii wa muziki wa kizazi kipya, Rajabu Kahal, maarufu Harmonize, na tayari limeshawahoji watu sita.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari, akibainisha kuwa mpaka sasa waliohojiwa ni Frida Masanya (36), Kajala, na mtoto wake Paula Peter (18).

Wengine aliwataja kuwa ni wasanii wa kundi la WCB; Raymond Mwakyusa (27), Rayvann na Claiton Revocatus (34), Babalevo.

Alisema wengine ni Catherine Charles na Juma Haji ambao wote walikamatwa na kuhojiwa kwa nyakati tofauti na kupewa dhamana juzi jioni.

"Harmonize alitoa malalamiko baada ya kusambazwa kwa picha hizo na watu ambao hawamtakii mema katika shughuli zake. Taratibu za upelelezi zinaendelea, tukikamilisha jalada litapelekwa kwa wakili wa serikali wa kanda ili kuyapitia kama kuna jinai wafikishwe mahakamani," alisema.

Kamanda Mambosasa alitoa onyo kwa watumiaji wa simu na mitandao ya kijamii na kuwataka waheshimu matumizi yake na mila na tamaduni za Kitanzania.

"Hata kama mtu anatoka bafuni ukampiga picha akiwa hajajisitiri vizuri, ni kinyume cha maadili ya Mtanzania, halafu unaitupa kwenye mitandao ya kijamii, ni makosa kisheria, sheria inayokabiliana na makosa ya kimtandao," alionya.

Aliwataka Watanzania kujiepusha na matumizi hayo ya mitandao ya kijamii ambayo hayana afya na ustaarabu.

Alisema wasanii wamekuwa watumiaji wabaya wa mitandao kwa kurushiana mambo ya kutaka kushusha nafasi ya mwingine kimuziki kwa sababu ya makundi waliyonayo.

"Ninawaonya wasanii, tunawaheshimu sana, ni kada nzuri inafanya vizuri na ni sehemu ya ajira kupitia kazi zao, waheshimu ajira zao, waheshimu kazi zao, waheshimiane na kila wanachotaka kukifanya wajiulize 'kwa kufanya hili sijavunja sheria ya nchi?'

"Ukikuta unaivunja, basi ahirisha, hatutamwangalia mtu kwa heshima yake, kwa nafasi yake. Akitenda kosa, atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria kama wahalifu wengine," Kamanda Mambosasa alionya.

# Tarehe ya safari treni SGR yatajwa

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema safari za treni ya kisasa kutoka Pugu, Dar es Salaam hadi Morogoro zinatarajia kuanza Agosti, mwaka huu.

Majaliwa amesema ujenzi wa kipande hicho cha Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kimekamilika kwa asilimia 91.

"Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), imetupa faraja, kwamba kufikia mwezi wa nane mwaka huu, tunaanza kuungurumisha treni yetu ya umeme kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro," Majaliwa alisema jana mkoani Dar es Salaam.

Alisema hakuna mradi wowote ulioanzishwa katika awamu ya tano ambao utakwama.

"Ninataka nitumie nafasi hii kuwathibitishia Watanzania kwamba, miradi yetu yote mikubwa ambayo ilianzishwa awamu ya tano ambayo tunaendelea nayo awamu ya sita, tutaendelea nayo na tutahakikisha inakamilika na inatoa huduma, nimezungumza haya mara nyingi na nitaendelea kusisitiza.

"Kwamba usimamizi wetu hautateteреka, mfumo wetu ni ule ule na pale ambapo hapaendi vizuri, hapohapo tunakemeana. Tunataka fedha ambayo tunaitumia ya Watanzania kuiweka kwenye miradi, itumike mpaka sarafu ya mwisho. Ninataka niwatoe hofu wananchi kwamba miradi yetu yote itakamilika na wasitarajie kwamba kuna mradi utakaokwama.

"Ninawasihi Watanzania tuendelee kushirikiana na kuwa wamoja, tusimamie miradi yetu, tuisemee miradi yetu, kama kunakuwa na mpotoshaji, mwambieni ukweli, asiwakatishe tamaa Watanzania.

"Tumepanga, tunatekeleza na tunataka miradi ifanye kazi kwa wananchi. Lakini pia tunawajibika sana kuhakikisha kwamba nchi hii inabaki kuwa ya utulivu na amani.

"Tumeshagundua siri ya mafanikio. Kumbe nchi tukiamua kufanya kazi wakati wa kazi na tukaacha mambo mengine ambayo yanaingilia shughuli za kazi, tunapata mafanikio makubwa. Tusiruhusu mambo mengine ambayo yanatufanya tusifanye kazi, tusimamie kila mtu afanye kazi ili tupate mafanikio. "Hatua tuliyofikia ni nzuri na tunaendelea vizuri tu, hatutarajii mtu mwingine aingie hapa aanze kutuvuruga tena, tunatarajia nchi yetu tupate mwelekeo mzuri na iendelee kuwa mfano wa kuigwa na mataifa mengine," alisema.

Kuhusu Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Majaliwa alisema wanatarajia kupata timu ya watu watakaousimamia mradi kwenye nafasi na heshima yake.

"Jana (juzi) tulikwenda kwenye mradi wa DART ambao hauendeshwi vizuri, lakini mradi huu umekuwa ni mfano na kuna nchi ambazo zilikuja kujifunza kwetu, sasa haiwezekani nchi zinakuja kujifunza kwetu halafu tunaanza kuharibu.


## CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

# TANGAZO

## MAFUNZO YA UONGOZI NA MAADILI

Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), kinapenda kuwatangazia kuwa kutakuwa na Mafunzo maalumu ya Uongozi na Maadili yatakayofanyika kwa muda wa wiki moja. Lengo la Mafunzo haya ni kuwajengea uwezo washiriki katika stadi za Uongozi, Maadili na utawala bora na kuwajenga katika misingi imara ya Uongozi bora, uwajibikaji na uzalendo katika taasisi zao za Umma na binafsi kwa manufaa ya Taifa la Tanzania.

**Malengo mahususi ya Mafunzo**

i. Kujenga uelewa wa nadharia ya maadili na utawala bora na misingi ya utumiaji wa uelewa huo katika maeneo ya kazi.
ii. Kuboresha weledi wa washiriki katika kutatua migogoro na kufanya makubaliano ya kidiplomasia sehemu za kazi.
iii. Kuendeleza uwezo wa kufanya maamuzi kama viongozi na kupanua kiwango cha uelewa wa maadili na utawala bora kwa Washiriki.

**Walengwa**

Viongozi, Viongozi tarajali pamoja na Watumishi walio katika nyadhifa mbalimbali za kiuongozi katika taasisi za umma na binafsi.

**Muda wa Masomo**

Mafunzo yataendeshwa kwa muda wa wiki moja ambapo Mshiriki atachagua awamu moja kati ya nne kama ifuatavyo:

| Tarehe ya kuanza | Tarehe ya kumaliza | Mahali | Cheti kitakachotolewa |
|---|---|---|---|
| 3/5/2021 | 7/5/2021 | Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi na Maadili |
| 2/8/2021 | 6/8/2021 | MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi na Maadili |
| 23/8/2021 | 27/8/2021 | MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi na Maadili |
| 6/9/2021 | 10/9/2021 | MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi |

**Ada ya Mafunzo**

Gharama ya Mafunzo haya ni TZS 500,000/ ambayo italipwa kabla ya Mafunzo kuanza. Baada ya malipo, fedha haitaweza kurejeshwa.

**Jinsi ya kutuma maombi**

Maombi kwa ajili ya kuhudhuria Mafunzo haya yako wazi kuanzia sasa.
Mwombaji atatuma maombi yake kwa njia ya mtandao kwa kujaza fomu iliyokatika tovuti ya Chuo ambayo ni: www.mnma.ac.tz.
Mwisho wa kutuma maombi kwa ajili ya Mafunzo haya itakuwa ni wiki moja kabla ya tarehe husika ya kuanza kwa mafunzo.

**Mawasiliano**

**Kwa mawasiliano zaidi kuhusu programu hii maalumu ya Uongozi na Maadili unaweza kuwasiliana na Mratibu wa Mafunzo ya Uongozi na Maadili kupitia namba ya simu ya mkononi 255(22)2820041/47 au +255675337734: email: phillip.daninga@mnma.ac.tz au rector@mnma.ac.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkuu wa Chuo**
**Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

# Dk. Mwinyi ataka mabadiliko sheria kandamizi kwa wajane

**Na Mwandishi Wetu**, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameeleza haja ya kurekebishwa sheria kandamizi ambazo zimekuwa zikiwakosesha haki za msingi wajane.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipokutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa Jumuiya ya Wanawake Wajane Zanzibar (ZAWIO), walipofika Ikulu jijini Zanzibar.

Alisema ni vyema jumuiya ikawa na mapendekezo yatakayosaidia kubadilisha sheria ili kuondosha upungufu uliopo katika jamii ambao umekuwa ukiwasibu wajane.

Rais alisema si jambo la busara mwanamke kuachwa katika ndoa na kuachiwa watoto akihangaika nao bila kupewa msaada wowote wa kukidhi maisha yake.

Alisisitiza kwamba wako wanawake ambao huchuma mali na wenza wao na mara wanapoachana hawaambulii chochote jambo ambalo alisema si busara licha ya baadhi ya wanaume kutoa visingizio vya kidini kitu ambacho si sahihi.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Rais Mwinyi alisema yuko tayari kutekeleza mabadiliko ya sheria ili zisikandamize upande mmoja.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Uongozi wa Taasisi ya Wajane Zanzibar (ZAWIO), ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi hiyo ambae pia ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Tabia Makame Mohammed, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

Rais Mwinyi aliipongeza ZAWIO kwa kazi nzuri ya kujitolea katika kuwasaidia wajane katika jamii Unguja na Pemba na kuongeza kwamba kazi wanayoifanya viongozi wa jumuiya hiyo malipo yake yanatoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwa ni kazi kubwa na inahitaji moyo.

Kutokana na juhudi hizo, Dk. Mwinyi alitoa Sh. milioni 10 kwa ajili ya kuendesha ofisi ya jumuiya hiyo pamoja na vyakula vya futari kwa ajili ya wajane 300 walio katika mazingira magumu zaidi.

Rais Mwinyi alisema serikali itahakikisha inaiunga mkono ZAWIO katika kufikia malengo yake na kusisitiza kwamba yako mambo matatu makubwa ambayo yanahitajika katika kuimarisha taasisi hiyo ambayo ni soko, mtaji na elimu ya ujasiriamali.

Aidha, Dk. Mwinyi alieleza azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuiunganisha mifuko yake yote ili iwe rahisi kuyashughulikia makundi yanayohitaji huduma kwa ajili ya kuendesha shughuli zao.

Alisisitiza kwamba tayari serikali inalisimamia jambo hilo huku taasisi binafsi zikiwamo benki ambazo zimeanza kuunga mkono juhudi hizo ikiwamo CRDB ikiisaidia jumuiya hiyo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya ZAWIO, Mgeni Hassan Juma, alieleza juhudi zinazochukuliwa na jumuiya hiyo huku akiahidi kuhakikisha marekebisho ya sheria husika yanatekelezwa katika Baraza la Wawakilishi.

Mwenyekiti huyo ambaye pia ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, alimpongeza Dk. Mwinyi kwa kuiunga mkono jumuiya hiyo huku akimpongeza Mama Mariam Mwinyi kwa kuilea na kuisaidia.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa ZAWIO, Tabia Makame Mohamed, alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kuijali na kuiunga mkono jumuiya hiyo pamoja na kuthamini juhudi zake.

DANISH REFUGEE COUNCIL

TANGAZO LA ZABUNI

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUNUNUA BIDHAA/VIFAA KWA ZABUNI ZIFUATAZO.

1. ITB-TZA-004232 VIFAA VYA KUTENGENEZEA MKAA MBADALA
2. ITB-TZA-004234 VIFAA VYA KUCHOMEA TAKA ZA MKAA MBADALA

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAARIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 21.04.2021 HADI TAREHE 04.05.2021 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255627428470 au barua pepe jackson.maseke@drc.ngo

ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 06.05.2020 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.

UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@drc.ngo AU KULETA MOJA KWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI

# NEC yashtukia undugu vituo kupigia kura

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

KAMISHINA wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Omar Ramadhani Mapuri, amewataka wasimamizi wa chaguzi ndogo za ubunge na udiwani kuacha kuweka ndugu na jamaa zao vituo vya kupigia kura kusimamia ili kuondoa malalamiko.

Mapuri aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya siku tatu ya watendaji wa chaguzi ndogo katika kanda tatu wilayani Kahama.

Alisema kuwa kuweka ndugu au jamaa kwenye usimamizi wa vituo vya chaguzi kunasababisha athari kwa kuwa ni vigumu kuwachukulia hatua wanapoharibu kazi.

Aliwataka watendaji hao kuzingatia sheria na taratibu za uchaguzi katika maeneo yao na kufahamu jiografia ya sehemu unapofanyika uchaguzi.

Mapuri alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo ili kujua utaratibu na sheria za uchaguzi badala ya kufanyakazi kwa mazoea.

"Mmeaminiwa kwa kuwa mna uwezo, mnajiamini na kujitambua, kwa hiyo tuna imani uchaguzi utafanyika vizuri bila kuwa na dosari yoyote na kuhakikisha hakutakuwa na malalamiko yoyote kutoka kwa wananchi na vyama vyote vya siasa vitakavyoshiriki chaguzi ndogo hizi," alisema Mapuri.

Ofisa uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Nestory Anatory, ambaye atasimamia uchaguzi Kata ya Igusuke, alisema, watasimamia kazi hiyo kwa mujibu wa sheria.

Msimamizi wa uchaguzi jimbo la Kongwa mkoani Dodoma, Dk. Omary Nkulo, aliwataka wananchi kuwa watulivu na kujitokeza kupiga kura ili kutimiza haki yao ya msingi.

# Wabunge walia na bajeti TARURA

**Na Gwamaka Alipipi**, DODOMA

BAADHI ya wabunge wamelalamika kuhusu wanachokiita serikali kutenga bajeti kidogo kwa ajili ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), wakibainisha hatua hiyo inakwamisha utekelezaji wa miradi.

Katika mwaka wa fedha 2020/21, wakala huo ulitengewa Sh. bilioni 275.3 na hadi kufikia Februari mwaka huu, ulikuwa umepokea Sh. bilioni 172.85. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, TARURA imetengewa Sh. bilioni 627.04

Wakichangia bungeni hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka ujao wa fedha, wabunge hao walisema fedha zinazotolewa kwa ajili ya ujenzi wa barabara na madaraja ni ndogo.

Mbali na hilo, wabunge hao pia waliitaka serikali kuangalia upya mifumo ya TARURA ili kusaidia ufanyaji kazi.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Agness Marwa, alisema kutokana na kuwa na bajeti ndogo, TARURA imekuwa na mzigo mkubwa kutokana na miundombinu kuwa mibovu, hivyo si rahisi kufanya vizuri.

Mbunge wa Katavi (CCM), Sebastian Kapufi, aliitaka serikali kuongezea fedha wakala huo kwa kubuni chanzo mbadala cha namna ya kuongeza mapato, akisema kwamba fedha kidogo zimekuwa zikitolewa katika ujenzi wa barabara na madaraja.

Mbunge wa Segerea, Bona Kamoli (CCM), alisema kuna haja wakala huo uongezwe fungu ili kukidhi matarajio ya wananchi yaliyomo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inayotilia mkazo ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini na mijini.

HABARI KITAIFA

# Wabunge Dar wacharukia foleni, ubovu miundombinu

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

KUWAPO kwa ubovu wa miundombinu, foleni, mafuriko kila wakati Dar es Salaam kumewaibua wabunge wanaotoka katika mkoa huo, huku wakiishauri serikali kuhakikisha wanaelekeza nguvu katika utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP) awamu ya pili, ili kulinusuru Jiji hilo.

Wakichangia bungeni hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) mwaka 2021/21, wabunge hao walisema ubovu huo wa miundombinu umesababisha biashara nyingi kufungwa.

Mbunge wa Ilala (CCM), Mussa Zungu, alisema biashara zilizokuwapo Ilala nyingi zimekufa, wafanyabiashara wamefunga biashara zao na kukimbilia nje ya nchi kwa sababu ya ubovu wa miundombinu.

Zungu alibainisha kwamba Mradi wa DMDP awamu ya pili ni muhimu sana kwa taifa na kuiokoa Dar es Salaam ambayo inakua kwa kasi.

Alisema mradi huo haupo Dar es Salaam tu bali unatekelezwa nchi nzima na kwamba Dar es Salaam wanauita DMDP kwa sababu inaanza na D, lakini uko katika maeneo mengi nchini ikiwamo kwenye sekta ya umwagiliaji, kilimo.

Alisema serikali lazima ije na mikakati ya kuboresha miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam ambayo haipitiki hususani wakati mvua ikinyesha.

"Serikali ione umuhimu wa kuboresha hii miundombinu maana fedha zipo. Tubadilishe namna ya kutafuta kodi za Watanzania ili mapato yapatikane kwa wingi sana na yasaidie taifa," alisema Zungu.

Zungu alitoa ushauri kuwa wataalamu wa halmashuri nchini wepewe mafunzo ya ubunifu wa teknolojia ambazo zitaifanya nchi kukua zaidi kwenye visharia vya maendeleo ya watu..

Naye Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa, alisema ubovu wa miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam unawaongezea ugumu wa maisha wakazi wanaoishi pembezoni, kwamba wanalazimika kutumia fedha nyingi hususani nyakati za asubuhi na jioni kwa ajili ya usafiri kufika katika shughuli zao.

Alisema Jiji la Dar es Salaam (lilivyokuwa wakati huo kabla ya kuvunjwa), kwa muda mrefu limekuwa likiendeshwa pasipokuwa na mpango mkakati.

Alisema: "Tangu mwaka huu haikuboreshwa hadi ilipofika Juni mwaka jana ambapo serikali ilitangaza kwenye gazeti la serikali".

Silaa alisema hivi sasa Manispaa ya Ilala imekuwa Jiji na kwamba Temeke, Ubungo na Kinondoni ziko mbioni kuwa majiji.

Kutokana na hali hiyo, aliitaka serikali kuhakikisha majiji yajayo yanakuwa na miundombinu ya uhakika ili kuhakikisha wananchi wanafanya biashara vizuri na kuinua uchumi.

"Leo mvua ikinyesha Dar es Salaam barabara hazipitiki, maisha ya wakazi yamekuwa ya taabu. Mtu anatumia zaidi ya Sh. 1,000 ili afike mjini. Serikali iangalie umuhimu wa mradi wa DMDP. Miundombinu ya Dar es Salaam tunataka iboreke ili wananchi wafanye biashara na kukuza uchumi wa nchi," alisema.

Naye Mbunge wa Segerea, Bona Kamoli, alisema katika jimbo lake miundombinu ya barabara ni mibovu kwa muda wa miaka mitano.

Alisema barabara ya Vingunguti-Barakuda imesimama ujenzi wake na kusababisha wananchi waliokuwa wanaitegemea kupata matatizo. Pia alisema barabara ya Kimanga imejengwa kwa muda wa miaka mitano na bado haijakamilika.

"Huu mradi wa DMDP kuna hatihati kuwa umefutwa, Segerea tuna tatizo la bonde la Mto Msimbazi. Tulitoa ahadi ya kujenga kingo katika bonde hilo lakini hadi lae hatujaweka na mafuriko yanatokea, zaidi ya wananchi 40,000 wanakimbia makazi yao," alisema.




Rais wa Klabu ya Rotary ya Dar es Salaam (RCD), Nirmal Sheth (wa tatu kulia), Mkurugenzi wa Miradi wa klabu hiyo, Kumail Manji (wapili kulia) na Meneja Masoko wa SBC, Jasper Maston, kwa pamoja wakikabidhi moja ya madawati 250 kwa Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Tabu Shaibu (wa nne kushoto), jijini humo hivi karibuni, kwaajili ya Shule ya Msingi Zavala ambapo jumla ya madawati 410 yametolewa na klabu hiyo pamoja na wadau mbalimbali kwa lengo la kuhudumia wanafunzi 1430 katika manispaa hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataja sababu vifurushi kumalizika kabla ya muda halisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Dk. Faustine Ndugulile, amesema malalamiko ya wananchi kuhusu vifurushi kuisha kabla ya muda inasababishwa na mifumo iliyomo kwenye simu husika na si kwamba wanaibiwa na kampuni za simu.

Dk. Ndugulile aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao chake cha robo tatu ya mwaka na taasisi zilizo chini ya wizara hiyo kupitia mapato na matumizi kwa kila taasisi.

Alisema suala la vifurushi kuwashwa kabla ya wakati kisababishi ni vitu vilivyomo kwenye simu ambazo wananchi wanazinunua.

"Kuna simu zingine zinafanya 'automatic updating' au kuboresha mifumo yake ya uendeshaji na wakati mwingine inatumia 'data' kwa hiyo kama hujaweka 'setting' vizuri kila 'update' inayokuja kwa kila 'application' unayotumia inatumia 'data'.

"lakini wengine tunatumia mitandao ya 'whatsap' na kule hujaweka 'setting' ya kuzuia picha zisiji- 'download'. Kwa hiyo ukiwa na mitandao 100 au 1,000 picha zote zile zinaingia kwenye simu yake na zile zinatumia data," alisema.

Waziri alisema ni vyema elimu itolewe kwa wananchi ili mtu asione kama ameibiwa kifurushi kumbe simu yake mwenyewe ndiyo inafanya kazi hiyo.

Hata hivyo, ameagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC) kufanya ufuatiliaji wa malalamiko ili kuhakikisha kero za wananchi zinazohusiana na masuala ya mawasiliano zinashughulikiwa kwa wakati.

"Nimeagiza katika kila kikao cha robo mwaka walete taarifa ni malalamiko mangapi yalipokelewa, mangapi yameshughulikiwa na yapo hayajatatuliwa na kwa sababu gani," alisema.



MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bunge lisimame katika nafasi yake

**KATIBA** ya Tanzania imeweka bayana madaraka ya Bunge kuwa ni kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti, kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa.

Pia kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo. Mengine ni kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo sheria, na kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Kwa maana nyingine, serikali inawajibika kwa Bunge, ambalo wajibu wake ni kuifuatilia ikiwamo kuikosoa na kuishauri. Haya ndiyo matarajio ya wananchi ambao wanawakilishwa bungeni na wabunge wanaotokana na kuchaguliwa majimboni, viti maalum na viti 10 vya rais, ambao kwa pamoja wanapaswa kuhakikisha wanawasemea wananchi kwa yale yanayowagusa.

Hivi karibuni, badala ya Bunge kujikita kwenye mjadala wa hoja iligeuga kuwa mashambulizi dhidi ya aliyetoa hoja, huku kukiwa na pande mbili za kujadili uongozi wa rais wa tano dhidi ya uongozi wa rais wa sita.

Rais Samia Suluhu Hassan bila kumumunya maneno alisema mwenendo wa Bunge hauridhishi na mjadala wa kulinganisha watu hauna afya kwa taifa, huku akiwataka kujikita katika kujadili bajeti.

Kama ambavyo ameona, wananchi ndiyo wenye maumivu zaidi kwa kuwa katika matatizo yao wanataka kusikiliza mbunge wao atasema nini na serikali inajibu nini ili kumpa tumaini la maisha.

Kuna mihimili mitatu ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama ambayo inategemeana na ni lazima ishirikiane kufanya kazi, huku kila mmoja ukiwa na nguvu kisheria, lakini inapofikia hatua muhimili mwingine (serikali) unaona mwingine hauenendi katika mstari basi kuna tatizo kubwa na ni lazima hatua za kujisahihisha zichukuliwe.

Wananchi wanaamini wamechagua watu watakaobeba dhamana ya kuwasemea na siyo kubeba ajenda binafsi na kurushiana maneno ya kijiweni, bali kushindana kwa hoja ambazo zinajikita katika majukumu yao na kupaza sauti dhidi ya mahitaji ya wananchi.

Namna pekee ya wananchi kushiriki kupanga bajeti ya nchi au mjadala wa bajeti ni kupitia kamati za maendeleo za kata (WDC), ambazo huibua vipaumbele kutoka kwenye vitongoji na mitaa, na baadaye baraza la madiwani la halmashari au manispaa, kisha kikao cha ushauri cha mkoa ambacho hujadili na kupitisha bajeti za wilaya.

Baada ya hapo ni ngazi ya wizara na kisha huingia bungeni kwa ajili ya mijadala ambayo inaweza kubadilisha jambo kwa kuongeza, kupunguza au kuhamisha bajeti ili kupata kitu kinachostahili na chenye manufaa kwa umma.

Inapotokea bunge linaondoka kwenye mstari wake wanaoumia ni wananchi kwa kuwa hakuna wa kuwasemea matatizo yao, na lazima watakuwa na wasiwasi na uwakilishi katika muhimili huo muhimu.

Ni vyema Bunge likajikita kujadili hoja muhimu ambazo zinagusa maisha ya wananchi moja kwa moja, na likasimama kwenye nafasi yake kuisimia serikali, badala ya kutimia muda katika mashambulizi ya maneno yenye kuudhi watazamaji na wasikilizaji, kwa kuwa sicho walichotumwa na wakumbuke tu wanalipwa kwa kutumia fedha za wavuja jasho, ambao wanataka kuona ahueni ya maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wanawake wabadili mbinu kusaka usawa wa kijinsia

Na Sabato Kasika

**WANAWAKE** katika uongozi, wanatajwa kuwa ni chachu kuifikisha dunia kwenye usawa ndiyo maana kwa muda mrefu kinamama wanapigania kutaka kuwapo usawa kwenye ngazi mbalimbali za uamuzi ikiwamo bunge.

Miaka ya 1990, wanawake walikuwa wanafanya kazi nyingi, ujira kidogo, unyanyasaji, bila kupewa malipo wanayostahili ikilinganishwa na wafanyakazi wanaume, lakini waliibuka kudai usawa na sasa mambo yamebadilika.

Hatua hiyo iliifanya serikali kufanya jitihada za kuwawezesha kiuchumi kwa kuanzisha mfuko wa uwezeshaji kiuchumi ikiwa ni pamoja na mfuko wa maendeleo ya wanawake wenye masharti nafuu.

Jitihada hizo za kuwakomboa wanawake kiuchumi zimeendelea kuwapo, ingawa kwenye suala la usawa wa kijinsi katika uongozi, bado halijafikia uwakilishi wa 50 kwa 50 kama ambavyo kila wakati suala hilo limekuwa likipendekezwa.

Mkurugenzi wa asasi ya kiraia inayojishughulisha na ustawi wa wanawake na mabinti ya KIWOHEDE ya Dar es Salaam, Justa Mwaituka, anapozungumzia wanawake na uongozi, anafafanua kuwa uongozi upo katika nyanja zote, siyo wa siasa tu, hivyo anashauri jitihada hizo za kusaka usawa zianze nyumbani.

Anaamini kwamba, kufikia usawa wa kijinsia katika uongozi, kuna haja ya kuandaa miondombinu mbalimbali yakiwamo mafunzo kwa wanawake na hasa wa vijijini ili kujua haki zao na kuzisimamia.

Kwa maoni yake hayo yafanyike kuanzia vijijini, kwenye halmashauri, mikoa na taifa wanawake wengi zaidi watatambua watakuwa wanajua wajibu wao katika familia na jamii kwa ujumla.

Mwaituka anatamani kuona kunakuwa na uwakilishi mkubwa wa wanawake ndani ya familia, kwa maana kwamba, wanawake wawe viongozi kwa kuwa na sauti kuliko ilivyo sasa.

Kinachoshauriwa na mkurugenzi huyo ni sahihi, kwa kuwa mapambano ya kutafuta usawa wa kijinsia ni muhimu, kuanzia katika ngazi ya familia badala ya kukimbilia juu wakati chini hakujawa sawa.

Hivyo wakati wakitafuta usawa kwenye ngazi za uamuzi, ni vyema pia wakakumbuka kwamba si lazima wategemee siasa, bali wajikite zaidi kutafuta uongozi kuanzia ngazi ya familia kwanza ili kuondoa mfumo dume.

Nia siyo kuwakatisha tamaa, bali wakianza kumaliza mfumo dume kwenye ngazi ya familia watakuwa wameiva na kusaidia kusambaratisha mfumo huo kwenye ngazi nyingine za maamuzi.

Tangu harakati hizo zilipoanza, uwakilishi haujawahi kufikia 50 kwa 50 katika uongozi, kwa vile safari ya kufikia hatua hiyo bado ni ndefu, kwa kuwa hata katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana, wabunge na madiwani wanawake wa kuchaguliwa ni wachache ukilinganisha na wanaume.

Wengi wameendelea kuishia kuwa wabunge na madiwani wa viti maalum ambavyo wamekuwa wakivikitaa, ingawa wameshiriki katika mchakato wa kura za maoni, lakini wakaangushwa.

Wanawake wengi wanatamani kuwania nafasi za uongozi katika kata na majimbo, lakini bado wanaachwa nyuma na kujikuta wakiwa wasindikizaji au kuambulia viti maalum.

Hivyo wadau wa siasa watafakari kwa kina katika na kupata njia sahihi ya kulisaidia kundi hili kubwa ambao ni wazi lina mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa kuliko kuliacha nyuma.

Hapa kuna mambo mawili ya kufanya, wanawake kujikita zaidi kutafuta uongozi kwenye ngazi za familia ili kuondoa mfumo dume au nafasi za uongozi ziwe na mrengo za kijinsia.

Kwa mfano mkoa unaweza kuwa na majimbo 10, yagawanywe, matano kwa ajili ya wanawake na matano mengine kwa ajili ya wanaume, hapo itakuwa rahisi kuwa na uwiano katika uongozi.

Hilo likifanyika, itakuwa ni rahisi mrengo wa kijinsia kufanya kazi, lakini vinginevyo, wanawake wataendelea kubaki nyuma kana kwamba hawana uwezo wa kuongoza na kumbe ni mfumo tu.

Ninashauri hayo kwa sababu zimekuwapo jitihada nyingi ambazo wanawake wamefanya kwa ajili ya kusaka usawa wa kijinsia katika uongozi hadi kufikia hatua ya kuandaa Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake, lakini bado lengo lao halijatimia.

Inapotokea hali kama hiyo, ni vyema wahusika kujipanga upya, aidha kwa kujikita katika kusaka uongozi kwenye ngazi ya familia au kukazania mgawanyo wa majimbo ama kata kwa mrengo wa kijinsia.

HABARI KITAIFA

# Marekani yajivunia mradi Tusome Pamoja

**Na Mwandishi wetu**

SERIKALI ya Marekani, kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imetumia zaidi ya Dola za Marekani Milioni 82 kwa mradi wa miaka mitano wa Tusome Pamoja, ukiwa na mradi wa miaka miwili wa hesabu na elimu jumuishi.

Hadi sasa, Mradi wa Tusome Pamoja umefikia zaidi ya watoto milioni 2.4 katika shule 3,060 na kuboresha umahiri wa kusoma, kuandika na hesabu.

Aidha, walimu 20,000 wamefundishwa mbinu za kufundishia za matamshi za kusoma na kuhesabu.

Mkurugenzi Mkazi wa USAID nchini, Andrew Karas, akizungumza na waandishi wa habari kwa njia ya mtandao, alisema Marekani inasherehekea miaka mitano ya mradi huo ambao umeleta mafanikio katika mikoa ya Ruvuma, Morogoro, Mtwara na Zanzibar na kuimarisha mfumo wa ujifunzaji kwa kuhusisha pia wasichana na wenye ulemavu.

Alisema lengo la hafla hiyo ni kuonyesha mafanikio endelevu katika usomaji, hesabu, na elimu jumuishi kwa sekta ya elimu ya awali na msingi.

"Elimu hutumika kama dira ya maendeleo mengine yote na hupunguza umaskini uliokithiri. serikali ya Marekani, USAID, itaendelea kushirikiana na serikali ya Tanzania kuhakikisha ufadhili ni muhimu kwa watoto na vijana wote wa Kitanzania, "alisema Karas wakati akifungua hafla hiyo kwa njia ya mtandao.

"Mradi wa Tusome Pamoja unaboresha kiwango cha ufundishaji wa stadi za msingi za madarasa ya awali, inaboresha njia za ufundishaji na ustadi, na inashirikisha wazazi na jamii katika kusaidia kuboresha matokeo ya elimu,"alifafanua.

Alisema miradi hiyo imeleta ufundishaji na mafunzo ya hesabu kwa walimu kujibu vizuri mahitaji ya watoto wenye ulemavu.

"Tunaamini kwamba ikiwa watoto wana afya, wamelishwa vizuri, wanasomeshwa, na wanasaidiwa na walezi wao na jamii, basi watakuwa na ujuzi unaohitajika kuwa vijana wenye tija, wenye nafasi nzuri ya kufuata na kufikia matarajio yao,"Alibainisha.

Kwa mujibu wa Karas, miradi yote miwili inashirikiana na Wizara ya Elimu Bara na Zanzibar, Taasisi ya Elimu ya Tanzania, Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na OR-TAMISEMI na OR-TAMISEMI-Idara Maalum.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, William Ole Nasha (Mb), akiongoza kikao kazi cha Menejimenti ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), wakurugenzi na wawakikishi wa wakurugenzi kutoka taasisi za Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kilichojadili kwa pamoja namna ya kuboresha mazingira ya uwekezaji, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mhadhiri adai mil. 130/- fidia mazingira magumu

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEKUWA Mhadhiri Mwandamizi katika Kitivo cha Sheria Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Dar es Salaam (TUDARCo), Dk. Lucas Kamanija, amemtaka mwajiri kumlipa fidia ya Sh. milioni 130 kutokana na kumtengenezea mazingira magumu akiwa kazini.

Dk. Kamanija amefungua shauri la madai katika Baraza la Usuluhishi wa Migogoro ya Kazi akiomba kulipwa fidia hiyo iliyomsababishia aache kazi katika chuo hicho.

Shauri hilo lilianza kusikilizwa juzi mbele ya Msuluhishi Edgar Fungo na pande zote mbili zilishindwa kufikia mwafaka na kutakiwa shauri hilo liende ngazi ya juu.

Shauri hilo lilifikishwa katika baraza hilo kwa ajili ya kutolewa uamuzi ambao ulishindikana kutokana na kiasi anachokidai Dk. Kamanija.

Wakili wa mlalamikaji uliongozwa na Nicholus Kashililika na Cheba Kameya na walalamikiwa wakitetewa na Wakili George Masoud.

Kashililika alidai kuwa Dk. Kamanija ambaye ni mmoja wa waazilishi wa kitivo cha sheria chuoni hapo, amefungua madai hayo katika baraza hilo akiomba kulipwa fidia ya kiasi hicho cha fedha baada ya kutengenezewa mazingira magumu yaliyomsababishia kuacha kazi.

Alidai wakati wakitafuta suluhu katika shauri hilo, hawakufikia mwafaka na mshauri Fungo kuwataka waende hatua za juu wakasikilizwe.

Kashililika alidai tayari wameshaanzisha mchakato kwa ajili ya kwenda ngazi ya juu, ili shauri hilo limpatie haki mteja wake.

Alidai mteja wake baada ya kuona mazingira magumu ya kazi aliandika barua ya kutaka kuacha kazi na uongozi wa chuo ulikutana naye na kuzungumza kuhusiana na madai yake ya fedha na kujulishwa atalipwa fedha zake aendelee na kazi.

Kashililika alidai kuwa Dk. Kamanija aliendelea na majukumu yake ya kazi na aliporejea nyumbani, mlinzi alimpelekea barua ya kufukuzwa kazi majira ya usiku hali ambayo ilimshinda kujibu barua hiyo kwa kuwa muda wa kazi ulikuwa umekwisha na siku inayofuata haikuwa ya kazi.

# Uzalishaji chanjo za mifugo watengewa fedha zaidi

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema itaendelea kutenga fedha za maendeleo kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya kuzalisha chanjo nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ( Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel), alisema lengo la kuimarisha miundombinu hiyo ni kuhakikisha kwamba chanjo zote 13 za kimkakati zinazalishwa na Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA).

Alisema katika mwaka ujao wa fedha, wizara hiyo imetenga fedha kwa ajili ya kununulia mashine kubwa zitakazotumika kupanua uzalishaji wa chanjo ili kukidhi mahitaji ya nchi.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa TVLA, Dk. Stella Bitanyi, alisema wanatarajia kuongeza chanjo ya saba ya homa mapafu (CCPP), na kwamba tayari imethibitishwa na maabara ya udhibiti wa chanjo za mifugo Afrika na kuwa na ubora wa viwango vinavyotakiwa kimataifa na kupewa cheti cha ubora.

Dk. Bitanyi pia alisema wanakusudia kupanua uwezo wa uzalishaji chanjo dhidi homa ya mapafu kwa ng`ombe (CBPP) kwa kuagiza mashine kubwa ya kugandisha chanjo.

"Lengo ni kuongeza uzalishaji wa chanjo hii ili kukidhi mahitaji makubwa ya soko, ndani na nje ya nchi. Na mashine nyingine kubwa imeagizwa kwa ajili ya kuchujia damu ya nguruwe ili kupata majimaji yanayohitajika katika uzalishaji chanjo ya CBPP na CCPP," alisema Dk. Bitanyi.

Pia, alisema wakala huyo kwa kushirikiana na wafadhili wakiwamo Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), wamefikia katika hatua nzuri kuelekea kupata ithibati kwa maabara za CIDB na CVL.

Dk. Bitanyi alisema mikakati mingine ni kuimarisha huduma za uchunguzi wa vyakula vya mifugo kwa kuongeza mashine mpya ya uchunguzi wa ubora ili kuhimili ongezeko la sampuli za vyakula vya mifugo.

Mikakati mingine alisema ni kuongeza uzalishaji wa chanjo ili kukidhi mahitaji ya nchi kutokana na kununua mashine muhimu ikiwamo kujaza, kufunika na kuweka lebo.




Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa Benki ya Absa Tanzania, Aron Luhanga (kulia) na Meneja wa Tawi la Absa Morogoro, Godfrey Chilewa wakikabidhi moja ya viti mwendo 20 kwa mwanafunzi mwenye ulemavu, Hassan Moyo (aliyekaa), vilivyotolewa msaada na benki hiyo, mkoani Morogoro jana. Viti hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 10 vitakabidhiwa kwa shule za msingi tano zenye wanafunzi wenye ulemavu katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Iringa, Mbeya na Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka TAKUKURU kuchunguza ujenzi zahanati

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

WANANCHI wa Kijiji cha Ulaya, Igunga mkoani Tabora, wameiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU ) kufanya uchunguzi wa matumizi ya Sh. milioni 30 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho ili kujua kwa nini haijakamilika mpaka sasa.

Ombi hilo lilitolewa na wananchi hao walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari kijijini hapo huku baadhi yao wakibainisha kwamba serikali ilitoa fedha hizo tangu mwaka 2019 baada ya zahanati hiyo kuungua moto hadi kuteketea.

Mmoja wa wananchi hao, Rehema Mussa, alisema pamoja na dhamira nzuri ya serikali kutoa fedha hizo ili kuwanusuru wananchi wake kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za matibabu, cha kusikitisha ni kwamba hadi sasa haijakamilika.

Alisema taarifa walizonazo ni kwamba baadhi ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya kazi hiyo zimeshatafunwa ndiyo maana zahanati hiyo haijakamilika kwa wakati, hivyo kusababisha huduma ya matibabu kwa wananchi kupatikana katika jengo la idara ya mifugo.

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao walitumia fursa hiyo kuiomba TAKUKURU kufanya uchunguzi wa haraka ili viongozi watakaobainika kuhusika na ulaji wa fedha wachukuliwe hatua.

Mmoja wa wafanyakazi wa idara ya afya anayefanya kazi katika zahanati ya kijiji cha Ulaya, Florencia Kupaza, alisema kutokana na kutokamilika kwa zahanati hiyo wamelazimika kutolea huduma kwenye jengo lisilokuwa na umeme.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ulaya, Emmanuel Tatoki, alipotakiwa kuzungumzia juu ya kutokamilika kwa jengo hilo, alikiri kutokamilika licha ya kupokea Sh. milioni 30 kutoka serikalini muda mrefu.

"Tulipokea Sh. milioni 30 kutoka serikalini lakini fedha hizo zote tulimpa mkandarasi, Petro Ndimila, ili akamilishe ujenzi wa zahanati lakini alisimama hadi sasa kutokana na kuumwa na hivi sasa anaendelea na matibabu mkoani Shinyanga," alisema.

Hata hivyo, alisema hivi sasa wanaangalia uwezekano wa jinsi ya kupata fedha zingine za kumalizia ujenzi wa zahanati hiyo na kuwataja waliosababisha serikali ya kijiji kumpa mkandarasi fedha zote kabla ya kumaliza kazi ni uongozi wa Idara ya Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kwa madai kwamba wanamwamini mkandarasi huyo.

Diwani wa Kata ya Ugaka, Emmanuel Cheyo, alisema kwamba walimpa kazi hiyo mkadarasi Februari 21, 2019 na kwamba Januari 2, mwaka jana walimkabidhi mkandarasi Sh. milioni 30 na kumtaka akabidhi jengo la zahanati hiyo Mei 20, mwaka 2020.

# Shule Mufindi zasaidiwa mil. 17/-

**Na Mwandishi Wetu,** MAFINGA

WILAYA ya Mufindi mkoani Iringa imewezeshwa kwa kupewa msaada wa Sh. milioni 17.3 kwa lengo la upatikanaji wa huduma za jamii.

Uwezeshaji huo umefanywa na Benki ya NMB kwa kutoa vifaa kadhaa vikiwamo madawati 50 kwa ajili ya Shule ya Msingi Upendo, viti 12 na meza 12 kwa ajili ya shule ya Isupilo na mabati 200 kwa ajili ya shule za msingi Nyamalala na Amani yenye lengo la kuezekea madarasa vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 17.3.

Baada ya kupokea misaada hiyo, mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Joseph Mchina, aliishukuru benki hiyo kwa kuendelea kuchangia shughuli za maendeleo wilayani humo.

"Misaada hii imekuja wakati mwafaka kwani itasaidia sana kupunguza uhaba wa madawati kwa shule zetu na pia kukamilisha baadhi ya madarasa ambayo yalikuwa yameshajengwa lakini nguvu zilikuwa zinahitajika katika kuezeka, nawashukuru sana NMB," alisema Mchina.

Mchina alisema kuwa ifike wakati wananchi waone umuhimu wa benki hiyo katika kujitoa kwao na zawadi pekee ni kuwaunga mkono katika kufungua akaunti na kutumia benki hiyo kupata faida zaidi ili nao watoe zaidi kwa jamii katika sekta mbalimbali.

Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu, Straton Chilongola, aliushukuru uongozi wa wilaya kwa juhudi zake za maendeleo ya wananchi ambao alisema ni wadau wakubwa kwa mafanikio ya benki ya NMB.

Alisema benki inatambua mchango wa serikali kwenye kuisaidia kuweka mazingira wezeshi ya biashara wilayani Mufindi

"Ingawa Serikali inafanya makubwa, sisi kama wadau tuna wajibu wa kuunga mkono juhudi hizi za maendeleo kwa kusaidia jamii kwani kupitia jamii hii hii, ndio imeifanya Benki ya NMB kuwa hapa ilipo na kubwa kuliko benki yoyote hapa nchini," Bwana Chilongola alinena.

Wanafunzi wa shule zilizosaidiwa walisema msaada waliopata ni motisha tosha ya wao kufanya vizuri kitaaluma. Walimu wakuu wao walisema mchango wa NMB si tu ni sehemu ya kurudisha fadhila kwa jamii lakini pia ni juhudi za kuboresha elimu nchini.

Meneja wa benki hiyo Tawi la Mafinga, Mary Mpasha, alisema kuwa ushirikiano unaotolewa unasababisha biashara ya NMB kukua zaidi hivyo kutoa faida kwa jamii inayowazunguka kama benki bora nchini kwa sasa na yenye matawi mengi zaidi.

# 'Ndugu nisaidieni kumpata mwanangu'

**Na Maulid Mmbaga**

MKAZI wa Salasala, Mariam Elias (17) (Pichani), amepotea katika mazingira ya kutatanisha tangu Novemba 11, 2020 akiwa nyumbani kwao.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Ayobu Alfonce, aliiambia Nipashe kuwa Mariamu alipotea akiwa nyumbani kwao Salasala mwisho wa lami na alikuwa na matatizo ya akili.

Alisema siku aliyotoweka aliruka ukuta wa nyumba na kutokomea kusiko julikana, licha ya juhudi za kumtafuta maeneo mbalimbali bila mafanikio.

"Baada ya Mariamu kupotea tulienda kutoa taarifa katika kituo cha polisi cha Salasala na tukapewa RB namba SLS/RB/663/20 na siku chache zilizopita tulipata taarifa kuwa kuna sehemu kaonekana ila tulipofika aliyemuona akatuambia kuwa amemponyoka na kukimbia," alisema.

Aliomba yeyote atakayefanikiwa kumuona ampeleke katika kituo cha polisi kilicho karibu naye au awasiliane naye kwa simu ya mkononi 0767230056 au 0713730954.

Aliwaomba wakazi wa mkoa huo na wananchi kuungana naye na kumsaidia kumtafuta mtoto kwa kuwa bado ni mdogo na kulingana na uhalisia wake si salama kuwa katika mazingira yasiyokuwa na uangalizi maalumu.

"Mariamu ni mtoto wa kike na tunakuwa na wasiwasi mkubwa kulingana na hali yake anahitaji uangalizi maalumu hivyo si salama kukaa katika mazingira hatarishi ninawaomba sana Watanzania wanisaidie kumtafuta mwanangu," alisema.



HABARI KITAIFA

# Wanafunzi wa kike wawezeshwa taulo 600

Na Lilian Lugakingira, BUKOBA

ILI kuhakikisha wanafunzi wa shule za msingi ambao wamekwishaingia katika mzunguko wa hedhi wanaendelea na masomo bila hofu, Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kagera limetoa msaada wa taulo za kike 600.

Taulo hizo zina thamani ya Sh. mil. 6.9 ambazo zitagawiwa katika shule za msingi tano zilizoko wilayani Muleba.

Akizungumza wakati wa kukabidhi rasmi taulo hizo, mwakilishi wa Meneja wa Kanda wa shirika hilo, Victor Nsiima, alisema taulo hizo zitaongeza mahudhurio na ufaulu kwa watoto wa kike, ambao wamekuwa wakikosa kuhudhuria masomo wanapoingia katika hedhi wakihofia kuchafuka na kuaibika mbele ya wanafunzi wenzao.

"Pia zitasaidia kuongeza uhuru kwa watoto wa kike katika kushiriki mambo mbalimbali wakiwa shuleni ikiwamo michezo, shule zilizonufaika ni Mayondwe, Kimbugu, Kagondo 'A' Kagondo 'B' na Bushumba," alisema.

Aidha Nsiima alisema kuwa mbali na taulo hizo pia World Vision wametoa madawati 440 yenye thamani ya Sh. milioni 33.7 kwa ajili ya shule za msingi nane zilizoko katika wilaya hiyo ambazo ni Bugasha, Kabuleme, Bushumba, Mayondwe, Kashumbilio, Kimbugu, Katoke 'A' na Katoke 'B'.

Akizungumza kwa niaba ya shule zilizopokea taulo hizo mwalimu wa taaluma katika Shule ya Msingi Bushumba, Davian Nyanto, alisema kuwa watoto wa kike wamekuwa wakikumbwa na matatizo mbalimbali pindi wanapoingia katika hedhi wakiwa shuleni, hali ambayo huwafanya wakati mwingine kushindwa kukaa darasani.

Akipokea msaada wa madawati na taulo hizo Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Richard Ruyango, aliwataka wanafunzi na walimu kutunza madawati hayo ili kuwanufaisha watoto wengine watakaokwenda baadae kupata elimu katika shule hizo.



Mkandarasi akiendelea na ujenzi wa daraja jipya la Tanzanite, linalounganisha maeneo ya Aga Khan Upanga Mashariki na Oysterbay kupitia Bahari ya Hindi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Polisi kusambaza muongozo wa uhalifu

Na Mwandishi Wetu

JESHI la Polisi limepanga kusambaza nakala za kijitabu cha Muongozo wa kufichua na kuzuia uhalifu kwa Polisi kata/shehia na maofisa watendaji wa kata/shehia, mitaa na vijiji kote nchini, ulioandaliwa na jeshi hilo.

Hayo yalisemwa na Kamishna wa Kamisheni ya Ushirikishwaji Jamii ndani ya Jeshi la Polisi, Dk. Mussa Ali Mussa kwa niaba ya Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, kwenye hafla ya kupokea nakala 4,000 za kitabu cha muongozo huo, katika ofisi ndogo za makao makuu ya jeshi hilo, Dar es Salaam.

Nakala hizo zimechapishwa kwa ufadhili ya Kampuni ya Kitanzania ya DataVision International iliyopo mkoani humo.

Dk. Mussa alisema kuwa jeshi hilo lilianza kupeleka miundombinu ya kiusalama katika ngazi za kata miaka nane iliyopita, lakini sasa linaboresha na kutoa muongozo ili kuhakikisha changamoto za kijamii zinapata suluhisho kwa ufanisi zaidi katika ngazi zote.

Alisema jeshi hilo lina imani kuwa kama wananchi na maofisa kata/shehia pamoja na viongozi wa ngazi za serikali za mitaa na vijiji wanapata muongozo mzuri wa kufichua na kuzuia uhalifu wanaweza kupunguza changamoto zinazopelekea uhalifu zilizopo katika jamii.

Aidha, Kamishna Dk. Mussa alisema kuwa maendeleo ya kiuchumi yanayoletwa na serikali yanaweza kushika kasi zaidi kama uhalifu utazuiwa katika ngazi zote.

"Serikali inajitahidi kuhakikisha kuna maendeleo ya kijamii... shule zinajengwa, miundombinu, madawa hospitalini. Haya yanafanywa ili kuona mambo mawili yanaenda sambamba, yaani uchumi na ustawi wa jamii vinaenda sambamba," alisema Kamishna Dk. Mussa.

"Sasa haya mambo mawili hayawezi kwenda vizuri, hayatakuwa endelevu kama kama hakuna mifumo mizuri ya ulinzi. Mifumo ya kiulinzi ndiyo itajenga ngome ya kuwapo maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Tunaweza kuwa na miundombinu mizuri lakini ikawa inahujumiwa na wahalifu," aliongeza.

Aidha, kwa niaba ya Inspekta Jenerali wa Polisi, aliishukuru Kampuni ya DataVision International kwa ushirikiano wake kama wadau wa ulinzi na usalama, kwani nakala walizochapisha zitasaidia katika kufikia wananchi wengi zaidi.

Akizungumzia Mradi wa Uboreshaji wa Sekta ya Ulinzi Binafsi kwa Njia ya Kielektroniki (PSGP), aliwataka wafanyakazi wa kampuni binafsi ya ulinzi kuendelea kujiandikisha kwenye kanzi data, kwani mradi huo ni mzuri na wao ndio waliouwasilisha kwa Jeshi la Polisi.

"Mradi upo na unaendelea, na sisi tunauunga mkono kwa asilimia mia moja. Wito wangu kwao ni kwamba waendelee tu kujisajili kwenye mfumo. Faida ya huo mradi kwa jeshi la polisi ni kubwa, lakini hata kwa wao. Kwa ufupi, tunajiandaa ili watu wa DataVision waje kufanya 'presentation' (uwasilishaji) ili tuone pale tulipofikia na changamoto ili tuendee na kazi. Hakuna kusimama. Tumeambiwa 'Kazi iendelee'," Dkt. Mussa aliongeza.

Naye Mkurugenzi wa Miradi kutoka DataVision International, Macmillan George, aliyekabidhi nakala hizo kwa Jeshi la Polisi; alisema kampuni hiyo imeungana na Jeshi la Polisi kwa kuchapisha nakala hizo kwa kuwa wao ni wadau wa ulinzi na usalama kwa kuamini kuwa, shughuli zote za kiuchumi zitafanyika na kufanikiwa endapo nchi itakuwa na usalama wa kutosha.

Alitoa wito kwa kampuni na wadau wa maendeleo kwa ujumla kuunga mkono juhudi za Serikali na Jeshi la Polisi katika kutoa elimu na kuimarisha ulinzi katika ngazi za Kata, Shehia, Kijiji na Mtaa.

## Daraja la Tanzanite lakamilika kwa 70%

Na Beatrice Moses

UJENZI wa daraja la Tanzanite linalokatiza ndani ya Bahari ya Hindi, linalotarajiwa kupunguza kero ya foleni kwa watumiaji wa Barabara ya Ali Hassan Mwinyi jijini Dar es Salaam, umekamilika kwa asilimia 70.

Mhandisi Kiongozi wa Kampuni ya Afrisa Consulting ambayo ni moja ya makandarasi, Samson Kundineza, akizungumzia kuhusu hatua hiyo wakati alipokuwa akizungumza jana na Idara ya Habari (MAELEZO), alibainisha kuwa licha ya ujenzi huo wa mradi wa Selander kufikia hatua hiyo pia umekuwa na manufaa kwa wahandisi waliomaliza vyuo kwa kuwa wamepata nafasi ya kujipatia uzoefu.

"Mradi huu umezalisha mafundi wazuri sana umesaidia wanafunzi na wahitimu wa uhandisi kujifunza na kuvuna uzoefu," alisema.

Alisema kuwa daraja hilo ambalo pia linaongeza aina ya vivutio vya utalii vilivyopo Dar es Salaam linajengwa ndani ya bahari na linagharimu Sh. Bil 243 litasaidia kuwezesha daraja la Selander linalovuka juu ya Mto Msimbazi kutoelemewa na magari hivyo kusababisha foleni.

Alisema kuwa watu wengi walikuwa wanashindwa kufika mahali wanapokwenda kwa wakati kutokana na foleni ambayo ilisababisha msongamano wa magari kwenye barabara kadhaa katikati ya jiji, ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Oktoba mwaka huu.

Awali Mhandisi Miradi wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Rajab Manger, alisema kuwa mradi huo ulianzishwa baada ya kubainika kuwa daraja la awali la Selander limezidiwa kutokana na wingi wa magari yanayopita hapo.

Mradi huo ulianza mapema mwaka 2018, baada ya kazi ya usanifu kukamilika hivyo kazi ya ujenzi ilianza kwa kuchimba msingi wa nguzo takribani 200 chini ya bahari na zipo nyingine kadhaa ambazo zimejengwa kwa juu.

Serikali iliamua kuanzisha mradi huo ikiwa ni hatua ya kupata suhuhisho na kutatua kero ya foleni jijini Dar es Salaam inayosababishwa na mambo kadhaa ikiwamo kuongezeka kwa wingi wa magari hivyo wa daraja lililopo sasa kuelemewa.

# SIDO yapewa bil. 4/- za kuendeleza ujasiriamali

BUNGE limeelezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2020/21, serikali imeshatoa Sh. bilioni 4.29 kwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo kwa wajasiriamali.

Shughuli hizo ni pamoja maendeleo ya teknolojia na ujenzi wa majengo ya viwanda kwa wajasiriamali wadogo.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani kupitia SIDO kutengeneza mashine zitakazosaidia kuchakata mazao ya wakulima kama vile mashine za kutengeneza chips za ndizi, muhogo, sauce za nyama, karoti, pilipili hoho, mbogamboga kwa gharama nafuu.

Akijibu, Naibu Waziri Kigahe alisema mkakati wa serikali ni kuendeleza viwanda hususan vidogo sana na vidogo vinavyolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

"Serikali imeendelea kulijengea uwezo SIDO ili kubuni na kuendeleza teknolojia mbalimbali kutokana na mahitaji," alisema.

Alibainisha kuwa SIDO lina vituo vya uendelezaji teknolojia katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Kigoma, Lindi, Iringa, Mbeya na Shinyanga kwa ajili ya kutengeneza mashine za kuchakata na kusindika mazao ya kilimo.

"Mashine hizo ni pamoja na za kutengeneza chips za ndizi, viazi na muhogo, kukausha mbogamboga na matunda, kusindika nyanya, karoti na pilipili kwa ajili ya achali kulingana na mahitaji," alisema.

Aidha, alisema aina ya mashine zinazotengenezwa zinapatikana katika tovuti ya SIDO na husambazwa katika mikoa yote ya Tanzania bara kupitia ofisi za SIDO.

"Licha ya SIDO kutengeneza mashine hizo, pia imekuwa ikitoa mafunzo ya usindikaji wa muhogo, ndizi, nyama, karoti, pilipili na mbogamboga katika mikoa yote ya Tanzania Bara," alisema.

Alisema bei za mashine hizo hutegemeana na uwezo wa mashine yenyewe na mahitaji halisi ya mjasiriamali.

"SIDO imeendelea kutafuta teknolojia mbalimbali za kisasa na nafuu ndani na nje ya nchi ili kuzitumia kutengeneza mashine kulingana na mahitaji ya wajasiriamali," alisema.

Vilevile, alisema SIDO inasimika mitambo ya kisasa yenye uwezo wa kutengeneza mashine kwa wingi na kusambaza kwa wananchi kwa gharama nafuu kwenye vituo vya kuendeleza teknolojia katika mikoa ya Kigoma, Lindi na Shinyanga.

"Naomba kutoa wito kwa wananchi wenye uhitaji wa mashine za kuchakata na kusindika mazao wakiwamo wananchi wa Jimbo la Vunjo kupitia Mbunge wao makini Dk. Charles Kimei kuwasilisha mahitaji yao kwenye Ofisi za SIDO zilizopo katika mikoa yote ya Tanzania Bara," alisema.

Alitoa rai kwa wabunge kuwahamasisha wajasiriamali kwenye maeneo yetu kutumia fursa ya uwepo wa vituo vya uendelezaji teknolojia (TDCs) vya SIDO ili kujinufaisha kiuchumi.



Mbunge wa Ilala, Musa Azzan 'Zungu', akichangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ya mwaka 2021/2022, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Vijana wasaidiwa kumudu ushindaji wa soko la ajira

OFISI ya Waziri Mkuu imetaja hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali katika kuhakikisha vijana wanamudu ushindani kwenye soko la ajira la ndani na nje ya nchi.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Latifa Khamis Juakali.

Mbunge huyo alihoji ni lini vijana wa Tanzania watapewa stadi mbalimbali za kuwaongezea ujuzi na maarifa kupitia mfuko wa uwekezaji wa wananchi kiuchumi.

Katambi alisema kwa kutambua umuhimu wa kuwapatia vijana ujuzi wa stadi za kazi na maarifa kama hatua mojawapo ya kuwawezesha vijana kumudu ushindani katika soko la ajira la ndani na nje, serikali kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi imetekelezwa.

Alibainisha kuwa kupitia program hiyo vijana 5,538 wamepatiwa mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya uanagenzi katika fani za ufundi stadi katika nyanja mbalimbali kupitia Taasisi ya Don Bosco na Vyuo vilivyo chini ya VETA.

"Serikali imeingia Mkataba na VETA wa kurasimisha ujuzi kwa vijana katika mikoa yote nchini katika fani za ufundi wa magari, useremala, uashi, upishi, huduma za vyakula na vinywaji, ufundi umeme, uchomeleaji vyuma, ufundi bomba, uchongaji vipuri na ushonaji wa nguo," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2020/21 kufikia Februari, 2021 jumla ya vijana 10,178 walikuwa wamerasimishwa na kati yao 28 ni Watu wenye Ulemavu na vijana wanaohitimu elimu ya juu wanaendelea kupata mafunzo ya uzoefu kazini ambapo serikali imeendelea na zoezi la kuwashikiza wahitimu kwa waajiri.

"Kwa mwaka 2020/21 hadi kufikia Februari, 2021, wahitimu 1,203 wa vyuo vya elimu ya juu na kati wamekamilisha mafunzo ya uzoefu kazini kupitia viwanda, taasisi na kampuni mbalimbali za sekta binafsi na umma nchini na wahitimu 2,037 wanaendelea kupata ujuzi na uzoefu katika taasisi binafsi na za umma na kati yao, wahitimu 92 ni watu wenye ulemavu," alisema.

Hata hivyo alisema programu zote za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinashauriwa kuhakikisha zinawajengea wadau wake stadi za ujuzi mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya program husika.

## Bil. 48/- kujenga vyuo vya VETA

SERIKALI imesema ilishatenga Sh. bilioni 48.6 kwa ajili ya kujenga vyuo 29 vya Ufundi Stadi (VETA) katika ngazi ya wilaya ambavyo kwa sasa vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.


Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbulu Vijijini (CCM), Flatei Massay.

Massay alihoji serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA katika Jimbo la Mbulu Vijijini ili vijana wapate ujuzi.

Naibu Waziri Kipanga alisema serikali inaendelea na mpango wa kujenga vyuo hivyo ikiwa na lengo la kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Mkoa na Wilaya.

"Katika Wilaya ya Mbulu kuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tango ambacho pia kinatoa mafunzo ya ufundi stadi. chuo hiki kinaendelea na ukarabati na ujenzi wa miundombinu utakaogharimu jumla ya Sh. milioni 605.2 ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021,"alisema.

Hata hivyo, alisema katika kipindi ambacho serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA wilayani humo, alishauri wananchi wa jimbo hilo kuendelea kutumia vyuo vilivyopo nchini, ikiwa ni pamoja na Chuo Cha Maendeleo ya Wananchi- Tango na Chuo cha VETA Manyara.




Habari zote na Augusta Njoji

Ni zama za kuhuisha uzalendo na fikra pevu za Muungano

Ukurasa 12





Ukurasa 13

**Mbunge anapowakumbuka wapigakura wake ...**



Ukurasa 14

**Rais 'kinda' anayetwishwa msalaba mzito wa Cossovo**

siasa

JUMATANO APRILI 21, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Rais anapokaripia wabunge...

## • Wadau wataka wajitafakari,kujipima

**Na Waandishi Wetu**

KAULI ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwataka wabunge kujadili maslahi ya nchi na siyo mipasho, inaelezwa kuwa ni maagizo ya kuliamsha bunge kujitafakari na kujihoji iwapo linafanya kazi yake ipasavyo.

Mwishoni mwa wiki, Rais alisema anaona kama mijadala bungeni inatoka nje ya kile kinachokusudiwa na kinachochojiri ni mashambulizi ya mtu dhidi ya mwingine, viongozi na kulumbana zaidi badala ya kuleta hoja na fikra za kuishauri na kuikosoa serikali.

Akizungumzia onyo hilo kwa wabunge, Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba, Bob Wangwe, anasema wawakilishi hao wa wananchi wanatakiwa wazungumzie maslahi ya nchi siyo hoja ambazo hazina manufaa kwa taifa.

Anasema kauli ya Rais inakuja ikitanguliwa na maoni ya wana harakati, asasi za kiraia na hata aliyekuwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali Profesa Mussa Assad, kuwa limeonekana kuwa lina udhaifu.

Anasema udhaifu huo unaanzia kwenye katiba kwa vile haijawapa wananchi mamlaka ya kuwawajibisha wabunge wanapoona hawatimizi wajibu ipasavyo au kufanya wapendalo.

Wangwe anasema udhaifu huo kikatiba unachangia wabunge kutojali na kufanya wapendalo kwa vile wanafahamu wapigakura hawawezi kuwafukuza na wana uhakika wa kudumu kwa miaka mitano.

"Kwa kuona upungufu huo, ni wakati wa serikali kuona umuhimu wa kurejea tena mchakato wa kuandikwa katiba mpya ili kuongeza uwajibikaji bungeni na kuwapa wapigakura mamlaka ya kuwaondoa wale wasiotimiza wajibu ..." anashauri.

Akizungumzia madai kuwa wakati wa bunge la vyama vingi, wapinzani walilichelewesha na kulikwamisha bunge kufanya uamuzi na mijadala inayohusu maendeleo ya nchi bila sababu kwa vile muda wote walipinga na kusoa, alisema : "Waliokuwa na hisia hizo sasa wameona kuwa upinzani unahitajika uwepo bungeni."



Wabunge pamoja na kutunga sheria wana jukumu la kushauri , kukosoa serikali na kupitisha bajeti yake. **PICHA: MTANDAO**

Anasema ni wakati wa serikali na wapigakura kuhakikisha kuwa kunakuwa na uwakilishi wenye maoni na mtizamo tofauti ili kuendeleza na kudumisha demokrasia na mijadala inayolenga kuikosoa, kuisimamia na serikali na kutetea maslahi ya nchi.

Anapoulizwa anadhani nini Rais Samia atakasema bungeni kesho wakati akilihutubia bunge, alisema anatarajiwa kutoa mwekeo wa taifa katika kipindi cha uongozi wake, ataeleza miradi inayokusudiwa kutekelezwa kuomba uungwaji mkono na wabunge.

**KUKUMBUSHWA WAJIBU**

Akizungumzia maelekezo ya Rais Samia kwa bunge, mbunge wa zamani wa Moshi Vijijini, Thomas Ngawaiya, anasema, amelenga kuwakumbusha wabunge kuzingatia wajibu wao wawapo bungeni.

Anasema, bungeni ni sehemu ambayo kuna mijadala ya hoja zilizo muhimu na zinazoletwa mbele yao, kupaza sauti za wapigakura, kusimamia na kuishauri serikali na siyo malumbano yasiyo ya tija kwa taifa.

"Bungeni si sehemu ya mipasho, matusi, kejeli, lugha ya kuudhi kama ambavyo baadhi ya wabunge wamekuwa wakifanya na ni jambo jema kuwa Rais ameliona hilo na kulikemea," anasema Ngawaiya.

Ngawaiya anasema, alikuwa mmojawapo wa watu waliokuwa wakikerwa na kile kilichokuwa kikifanyika bungeni na kwamba amefurahishwa na hatua ya Rais Samia kutuliza hali ya hewa mapema.

Mwanasiasa huyo anasema, kanuni za bunge haziruhusu mbunge kutumia lugha ya kuudhi, na kwamba alishangaa kusikia baadhi ya wabunge wakiambiana hawajasoma au wewe ni wa darasa la saba.

Anasema, kwa kuwa Rais anajiandaa kuhutubia bunge kesho , anaamini hotuba yake itakuwa na maelekezo mengi na kwamba, ataweka wazi misimamo mingi ya serikali yake na kile anachotaka kifanyike.

"Tutarajie makubwa katika hotuba ya Rais wetu ambayo yataligusa bunge na mengi na serikali yake kwa ujumla inayopanga kuyafanya kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii na watu wake," anasema.

Anaongeza kuwa anaweza kuwaweka sawa wabunge ambao wamekuwa wakienda nje ya mstari wanapochangia hoja bungeni na kusababisha malumbano yasiyo na tija kwa wapigakura wao na taifa kwa ujumla.

"Hadi rais kufikia kuzungumzia kilichokuwa kikiendelea bungeni, ni wazi hakufurahishwa nacho na ingawa si mtu wa kufoka, hatua hiyo inaonyesha hakupendezwa na uendeshwaji wa muhimili huo ambao pamoja na kutunga sheria, kupitisha bajeti na kuishauri serikali unawajibu pia wa kujiendesha kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu," anasema.

INAENDELEA UK.14

# Ni zama za kuhuisha uzalendo na fikra pevu za Muungano



Waasisi wa Muungano, Mwalimu Julius Nyerere na Abeid Amani Karume, wakitiliana saini hati za makubaliano. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

JUBILEI ya miaka 57 ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar imewadia wiki ijayo, kwa umoja wao Watanzania na Wazanzibari wanakumbuka tukio hilo la kuunganisha mataifa yao na kutazama mafanikio na changamoto ili kuuimarisha na kuudumisha zaidi.

Licha ya kuvuka mabonde na mito wengi wanautizama Muungano kama 'mboni ya jicho' la siasa za Tanzania na kwa ujumla wananchi wanakuwa waoga wa kuuzungumzia na kuelezea hisia zao.

Ni kweli kuwa japo Muungano umeishi kwa zaidi ya nusu karne unaogopwa kuzungumziwa na kwa miaka ya hivi karibuni sera za vyama vingi pamoja na kuandikwa kwa katiba mpya ambayo hata hivyo ilikwama , ndivyo vitu vilivyofungua mjadala, kuujadili hasa katika kikao cha Bunge Maalum la Katiba na kwenye kampeni za kisiasa.

> “Wazanzibari na Watanzania Bara wanataka Muungano uwape haki za kichumi ili kumiliki, kutumia na kunufaika na ardhi, madini.

Wakati Jumatatu ijayo Muungano unatimiza miaka 57 ni wakati wa kuufanya Muungano uwe wa wananchi, usiiogopwa wala kuhofiwa kwa kuunda mamlaka maalumu ya kuusimamia na kuuendesha unapoingia kwenye hatua nyingine ya maisha au kufikia miaka mia au Jubilei ya miaka 100.

Leo majukumu ya Muungano yako ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais, eneo linaloshughulikia pia Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, pengine kuna haja ya serikali ya awamu ya sita kuwa na chombo mahsusi cha kuusimamia Muungano na chenye dhamira ya dhati ya kutengeneza mazingira ambayo yatawafanya Watanzania kuupenda, kuuheshimu, kuujadili, kuukubali na pia itakuwa inaangalia matakwa ya wananchi kuhusu umoja huo kwa kutizama kila Wazanzibari na Watanzania Bara wanachokitaka.

Ni wazi kuwa kukiwa na chombo au mamlaka ya kuendeleza Muungano itatekeleza majukumu yake kwa utashi wa kisiasa na siyo kufanya mambo kwa mtindo wa mazoea ili kutimiza lengo la kuhakikisha kuwa unadumu na kuuleta karibu na wananchi.

Muungano utadumu na utaendelea kuwapo kwa sababu serikali imetekeleza kile wananchi walichokitaka na hasa kuona umoja na mshikamano wa mataifa hayo, unaboresha maisha yao au kwa maana nyingine watu hawataki siasa, wanapenda mabadiliko na maisha bora.

Kazi za chombo hicho endapo kitaundwa ziwe ni kuhakikisha kuwa Muungano unabaki kuwa jicho linalowalinda na kuwanufaisha mamilioni ya wananchi ambao hawana chama wala hawajui vyama vya siasa vinafanyakazi zipi, bali wanataka kuona maendeleo.

Ndani ya Muungano kinachotakiwa ni kukumbuka kuwa Watanzania wengi wanachotaka ni kupata haki zao za msingi za kiuchumi, kijamii na fursa za kuendesha maisha yao kwa mfano, mkulima anataka ardhi ili azalishe.

Wavuvi walioko Kizimkazi, Bagamoyo, Rufiji na Kojani wanapenda kuona miundombinu na teknolojia ikiwawezesha kuvua ndani ya bahari kuu na kuinua maisha yao wakati wafanyabiashara wanapenda kuuza na kununua kutoka Zanzibar, Tanga, Arusha na Pemba bila kusumbuliwa na mamlaka za mapato iwe TRA au ZRB.

Wazanzibari na Watanzania Bara wanataka Muungano uwape haki za kichumi ili kumiliki, kutumia na kunufaika na ardhi, madini, bahari na rasilimali zote za ardhini na majini ili waendeshe maisha yao na wapunguze umaskini.

Mamlaka ya kusimamia Muungano itakayoundwa ihakikishe kuwa unajaa maslahi ya wananchi si kuonekana kuwa ni chombo chenye matakwa au maoni ya kundi Fulani na kusababisha imani kuwa wanaonufaika ni upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano.

Watanzania Bara na Wazanzibari wangependa kuona nchi ikisonga mbele kwa kuhakikisha kuwa hakuna mwenye dhamira ya kuvunja Muungano wala kuupinga kwa vile umedumu kwa zaidi ya miaka 50 wakiukubali na kujivuna kuwa ni watoto wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Kuwapo kwa mamlaka ya kusimamia Muungano kutaendeleza umoja na kuepusha hisia za kuujadili kwa itikadi za vyama kwa kuwa chombo hicho kitakachokuwapo kisheria na katiba ndicho kitakachotoa mwelekeo na uhalali wa kisiasa wa kuwapo kwa umoja huo unaoziweka pamoja Zanzibar na Tanzania Bara.

## Rais Samia Suluhu Hassan anapokaripia wabunge...

**INATOKA UK.11**

Mbunge huyo wa zamani ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), anasema, hotuba ya rais pia inaweza kujikita kwenye suala la utawala bora kwa kwa sababu, hatua yake ya kukemea yale yaliyokuwa yakiendelea bungeni, ni wazi anapenda utawala bora, hivyo ninaamini suala hilo litagusiwa pia.

**KUBADILI GIA**

Katika mjadala huo, mchambuzi wa masuala ya kisiasa Abdul-Karimu Atiki, anasema ni wakati wa bunge kujiongeza na kujua upepo umebadilika na kujielekeza kwenye mwelekeo mpya, ili kuwa na mijadala yenye tija.

Anawakumbusha wabunge kuwa katika awamu zilizopita kuna mambo yaliyofanyika ambayo wananchi wanayakubali na mengine wanayapinga, hivyo hakuna sababu ya kuyaibua na kuyajadili zaidi bungeni kwa sababu tayari yanajulikana yasiendelezwe kwa vile ni kupoteza muda.

“Wabunge waende na wakati wajue kuwa zama zimebadilika siyo kuendelea kubaki nyuma na kushikilia misimamo iliyopita,” anasema mchambuzi huyo.

Anasema kukumbushwa na Rais kunaonyesha kuwa pengine kuna walakini kwenye kutimiza wajibu wake kikatiba, hivyo muhimili huo ujikite kushauri, kuelekeza serikali masuala yenye tija yanayoleta maendeleo.

Akizungumzia ukosoaji uliotolewa na baadhi ya wadau kuwa bunge halina meno, anasema udhaifu unaozungumziwa ni hatua ya muhimili huo kushindwa kuiwajibisha serikali au taasisi zinazofanya makosa hasa yanayoibuliwa na ofisi ya CAG.

Anasema udhaifu unaonekana kwenye kushindwa kukemea na kuchukua hatua unapotajwa upungufu na badala yake kuendelea kunyamaza au kutokujali ndiko kunakofanya chombo hicho kionekana kuwa ni dhaifu.

Anakumbusha kuwa kusema bunge ni dhaifu au halina meno wakati mwingine si sahihi kwa vile haliwezi ‘kuiuma serikali’ bali wanaofanya hivyo ni wananchi wanaofanya maamuzi kutokana na kile wanachoona hakiwaridhishi.

“Wenye meno ni wapigakura siyo wabunge. Hata hivyo bunge ni la kichama linaundwa na vyama na kile chenye uwakilishi mkubwa ndicho kinachounda serikali.”

Atiki anaeleza kuwa wabunge hao wenye serikali hawawezi kuiondoa serikali yao madarakani ndiyo maana wakati mwingine linaweza kuitwa dhaifu lakini wanajua namna bora ya kuishauri na kuikosoa serikali yao.

Mchambuzi huyo anashauri wabunge kuibua hoja zenye tija, mitizamo na zenye kutetea maslahi ya nchi na ikibidi wakubali kunahitajika tija kwenye kutimiza wajibu huo.

UCHAMBUZI

# Mbunge anapowakumbuka wapigakura kwa namna hii

**Na Sabato Kasika**

- Awaambia anajipanga kurudi tena 2025
- Akiri kimya chake kina mshindo mkuu



Kangi Lugola enzi zake alipokuwa mbunge. **PICHA: MTANDAO**

KANGI Lugola, ni miongoni mwa waliokuwa wabunge wa CCM ambaye katika mchakato wa kupata wawakilishi wa chama hicho kwenye uchaguzi mkuu, vikao vya juu havikurejesha jina lake.

Kabla ya kura kupelea alikuwa Mbunge wa Mwibara mkoani Mara, kwa muda wa miaka 10, lakini baada ya kukosa nafasi hiyo, amekuwa hasikiki tena kwenye harakati za kisiasa, kwa waliokuwa wakifuatilia shughuli za bunge, watakuwa wanakumbuka misimamo, mbwembe na vituko vya kila aina, wakati akiwakilisha hoja za wapigakura wa Mwibara bungeni.

Mwanasiasa huyo alikuwa na uwezo wa kushawishi na hata ikiwezekana alitumia mbinu mbalimbali ikiwamo kuchekesha ili mradi hoja yake iungwe mkono na wabunge wenzake na wakati mwingine katika mwendelezo wa shughuli za bunge kuna wakati alidhani kwamba akiongea hivi hivi huku mtu akimwona akitoa hoja anaweza kumhurumia, ikamlazimu kumwomba idhini spika amruhusu avaae kifunika uso ali mradi tu asimuonee huruma waziri mtoa hoja.

Kitendo hicho kilimlazimu spika ama akubali au akatae kutoa idhini: "Mheshimiwa mimi naomba uniruhusu nivae 'kininja' ili nitoe niliyo nayo kwa sababu bila kufanya hivyo nitamuonea huruma waziri".

Amewahi pia kuongoza wabunge wenzake kuichachafya serikali hadi mawaziri kujiuzulu nyadhifa zao, akidhaniwa na wanachama wenzake kuwa ni msaliti, lakini akawa anafafanua kuwa anaisaidia serikali ili ijirekebishe.

"Hivyo vilikuwa ni baadhi ya vituko vya Lugola wakati huo akiwa bado hajateuliwa kuwa waziri, kwa mara ya mwisho aliiongoza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kwamba vituko vyake havikuishia hapo, bali hata alipokuwa waziri, aliviendeleza kivingine ikiwamo kutembea akiwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM na pia kusakata muziki katika hafla mbalimbali akijiachia na kuvuta macho ya watu wengi.

Mambo hayo na mengine mengi, yalimfanya jina lake kuendelea kusikika midomoni mwa watu mbalimbali wakiwamo waliofurahia vituko vyake na wengine kumkosoa, hata hivyo, baada ya kuondolewa katika nafasi ya uwaziri, mwanasiasa huyo hakusikika kama zamani, bali wakati wa mchakato wa ndani ya chama wa kusaka mgombea ubunge, ambao hata hivyo aliwekwa pembeni.

Baada ya mchakato huo uliofanyika mwaka jana, huku nafasi ya ubunge ikichukuliwa na Charles Kajege, Lugola hajasikika tena ambapo Nipashe iliamua kumsaka na kufanikiwa kumpata.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili, anasema, kimya kingi kina mshindo mkuu, na kwamba kunyamaza kwake hakumaanishi kuwa ndiyo amekwisha kisiasa, bali ana mambo mengi ya kufanya, kama anavyoendelea kuelezea msimamo wake huo...

**SWALI: Baada ya kuwekwa pembeni katika mchakato wa kuwakilisha chama kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka jana mbona umekuwa kimya sana? Uko wapi na unafanya nini? Au ndiyo umeachana na siasa?**

**JIBU:** Kimya kingi kina mshindo mkuu. Siyo kwamba niko kimya tu, bali ninajipanga upya kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Hivyo wale waliozoea kunisikia bungeni ama kwenye shughuli za serikali, na sasa hawanisikii, wajue kuwa nipo ninaendelea na shughuli za kilimo kama kawaida huku nyumbani kwetu Mwibara, lakini pia nikijipanga upya, kwani miaka mitano si mingi. Ninatarajia kuibuka kwa kishindo. Ni vyema kutambua kuwa uchaguzi wa mwaka 2020 umekwisha na ni lazima maisha yaendelee kama kawaida. Hivyo kimya changu si kwamba sipo.

**SWALI: Huoni kuwa miaka 10 ambayo amewahi kuwa mbunge inatosha na sasa uwaachie wengine ili nao wawe wawakilishi wa wananchi wa Mwibara?**

**JIBU:** Siyo kwamba ninalazimisha kuwa mbunge, bali wananchi wenyewe ndiyo wanaonitaka na hata katika kura za maoni ndani ya chama wajumbe walinichagua kwa kura nyingi, lakini jina langu likakatwa kwenye vikao vya juu vya chama, lakini ukweli ni kwamba wananchi bado wanapenda niwawakilishe.

**SWALI: Kwani ulipata kura ngapi katika mchakato wa kupata mwakilishi wa chama katika uchaguzi mkuu?**

**JIBU:** Katika mchakato huo, mimi na Charles Kajege tulifungana kwa kila mmoja kupata kura 173 huku wagombea wengine Cyprian Musiba kura 58 , Bituro Kazeri akipata kura 33. Lakini jina ambalo vikao vya juu vilirudisha ni la Kajege ambaye kwa sasa ndiye mbunge, ila nikuhakikishie kuwa panapo uzima, nitarudi ulingoni kuwania jimbo la Mwibara.

**SWALI: Kipi ambacho kinakupa uhakika kwamba ukirudi ulingoni unaweza kuchaguliwa tena kuwa mbunge wa Mwibara?**

**JIBU:** Zipo sababu nyingi, lakini nikuambie tu kwamba tangu kumalizika kwa mchakato ndani ya chama hadi uchaguzi mkuu, niko huku Mwibara, ninaendelea kushirikiana na wananchi katika shughuli mbalimbali zikiwamo za kijamii, na wananchi wenyewe wanasema wazi kuwa wanatamani siku moja kuniona nikirudi tena bungeni kuwawakilisha. Kwa kuwa wao ndiyo wapigakura, ninaamini kwamba mizengwe isipokuwapo katika uteuzi wa jina la mgombea nitashinda na nitakata kiu yao ya kutaka niwanie ubunge katika uchaguzi ujao.

> Mheshimiwa mimi naomba uniruhusu nivae 'kininja' ili nitoe niliyo nayo kwa sababu bila kufanya hivyo nitamuonea huruma waziri.

**SWALI: Una ujumbe gani kwa Watanzania mara baada ya kifo cha Rais wa Awamu ya Tatu, Dk. John Magufuli?**

**JIBU:** Ujumbe wangu kwa Watanzani hautofautiani na ule ambao Rais Samia Suluhu Hassan ameshautoa kwa taifa kuwa, tuendelee kushikamana na kuimarisha umoja, amani na utulivu. Tuwe wamoja zaidi bila kujali tofauti za itikadi za vyama vyetu, bali tuunganishwe na Utanzania, kwani hilo ni jambo la muhimu, na tumuunge mkono rais wetu ili aweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu, kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

JUKWAA LA UONGOZI

VJOSA OSMANI

# Rais 'kinda' anayetwishwa msalaba mzito wa Cossovo

Na Christina Mwakangale

BUNGE la Kosovo bila kusita limemtwisha mwanamama Vjosa Osmani, jukumu la kuiongoza nchi hiyo, pengine likiishangaza dunia kutokana na jinsi na umri wake mdogo.

Vjosa, mwenye miaka 38, anaingia kwenye rekodi ya kuwa miongoni mwa marais wachache wanawake duniani, akikabidhiwa jukumu hilo wakati wa uchaguzi uliofanyika Februari mwaka huu nchini humo, uliomhalalisha kuingia mamlakani, baada ya rais aliyekuwapo kujiuzulu.

Mtangulizi wake, Rais Hashim Thaci, alijiuzulu baada ya kukabiliwa na shutuma za uhalifu wa kivita.

Vjosa aliyeapishwa mwanzoni mwa mwezi huu alikula kiapo April 7, baada ya bunge kumuidhinisha kwa kura zinazohitajika. Wakati wa Pasaka Jumapili Aprili 4, mwaka huu, alipigiwa kura na kupata viti 71 kumuidhinisha kati ya viti 120 vilivyopo bungeni.

Ingawa amepewa jukumu hilo, ana changamoto ya kutokubalika na vyama vya upinzani na asasi za kiraia, vikidai kuwa kuwapo rais, waziri mkuu na spika wa bunge, kutoka chama kimoja, si demokrasia.

Vjosa anafurahia kuwa kiongozi anayewawakilisha vijana wa Kosovo, licha ya ukweli baadhi hawamkubali.

Katika moja ya hotuba zake, Vjosa, anapendekeza mazungumzo yawapo na Serbia, huku akiitaka Yugoslavia, kuomba radhi kwa kuhusika na vita kipindi cha 1998 hadi 1999, vita ambayo ilileta uhuru wa Kosovo, ilipofika mwaka 2008.

Hadi Septemba mwaka jana, Vjosa alikuwa kati ya maofisa wakuu wa chama tawala cha Democratic League Kosovo.

Mtangulizi wake, Thaci, anasubiria kesi kwenye mahakama ya dunia ya uhalifu wa kivita- ICC iliyoko huko The Hague, nchini Uholanzi, kuhusiana na uhalifu wa kivita, ingawa amekana mashtaka dhidi yake.



Rais wa Cossovo, Vjosa Osmani, muda mfupi baada ya kuchaguliwa kuongoza nchi hiyo. **PICHA: MTANDAO**

### KABLA URAIS

Vjosa Osmani-Sadriu anakuwa rais wa pili mwanamke wa Jamhuri ya watu wa Kosovo akiwa spika mstaafu wa Balkan anakuwa rais wa saba kwa kipindi cha miaka mitano.

Kabla ya kuingia madarakani, rais aliyemtangulia, Novemba mwaka jana, alitangaza kujiuzulu baada ya kushtakiwa huko ICC.

Mahakama ya Kimataifa ya ICC ilimshtaki juu ya uhalifu wa kivita wakati wa mzozo dhidi ya vikosi vya Serbia mwishoni mwa miaka ya 1990.

Mwanamama huyu alianza kuwa mwanaharakati tangu akiwa binti akiwa anasoma sheria huko Pristina na kisha shahada ya uzamili na nyinginezo nyingi akizipata kutoka chuo cha Pittsburgh, kilichopo Marekani.

> Kabla ya kuingia madarakani, rais aliyemtangulia, Novemba mwaka jana, alitangaza kujiuzulu baada ya kushtakiwa huko ICC.

Vjosa anaonekana kama mwanamke mtoa ushawishi kwa wanawake wengine hususan walipo Balkan.

Anakuwa rais mwanamke wa pili Kosovo baada ya Atifete Jahjaga, ambaye aliongoza taifa hilo kuanzia mwaka 2011 hadi 2016.

Rais huyo ni mama mwenye mume na mabinti wawili.

### MTANGULIZI WAKE

Hashim Thaçi (52), kiongozi wa zamani wa kisiasa wa kundi la waasi wa waliojitenga la UCK, alitawala maisha ya kisiasa ya Kosovo kwa miongo miwili.

"Kama nilivyoahidi, sitakubali kwa mazingira yoyote kwamba nifike mbele ya mahakama kama Rais wa Jamhuri ya Kosovo," anasema katika moja ya mkutano na waandishi wa habari.

"Kwa hivyo, kutetea uadilifu wa mamlaka ya Rais na Kosovo, pamoja na hadhi ya raia wake, ninajiuzulu kwenye wadhifa wa uongozi wa Jamhuri ya Kosovo," anasema kiongozi huyo akiwa anang'atuka.

Thaçi anasema kuwa hana hatia katika mzozo wa miaka ya 1998 hadi 1999, akituhumu mahakama ya kimataifa.

"Watu wengi Kosovo wanaona mzozo huu kama vita vya haki dhidi ya ukandamizaji wa Serbia.

"Hizi sio nyakati rahisi kwangu na kwa familia yangu, na kwa wale ambao wameniunga mkono na kuniamini katika miongo mitatu iliyopita ya kupigania uhuru, uhuru na ujenzi wa taifa," anasema Thaçi.

Licha ya msimamo hu Kosovo kulitawala mashtaka ya mauaji, visa vya watu kutoweka.

### UHURU WA KOSOVO

Kosovo ilijipatia uhuru kutoka Serbia, Februari mwaka 2008, ingawa Serbia pamoja na nchi nyingine ikiwamo China na Urusi hazilitambua hilo.

Kosovo ni nchi isiyokuwa na bahari 'landlocked' ikiwa katikati mwa nchi za Balkans, huku majirani zake wakiwa Serbia, Macedonia ya Kaskazini, Albania na Montenegro.

Pamoja na uhuru huo Yugoslavia inaiona Kosovo kama ni jimbo la Serbia. Licha ya kwamba ni nchi ndogo ndani ya Balkan iliyopo katika Ulaya ya Kusini Mashariki.

Kihistoria Kosovo iliwahi kuwa eneo ambako ufalme wa kwanza wa Serbia ulianzishwa wakati wa karne ya 12.

Kosovo ilikuwa kitovu cha Serbia hadi mwisho wa milki ya Serbia ya Kale iliyovamiwa na Waturuki.

Chini ya utawala wa Waturuki idadi ya Waserbia ilipungua kwa sababu wengi walikimbia ukandamizi wa Waosmani dhidi ya Wakristo.

Waalbania walihamia humo kutoka maeneo ya jirani yaliyokuwa pia sehemu ya Milki ya Osmani.

Katika karne ya 19 idadi kubwa ya wakazi wa Kosovo walikuwa tayari Waalbania.

Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia (WW II), Kosovo ilikuwa sehemu ya Jamhuri ya Serbia ndani ya shirikisho la Yugoslavia.

Tofauti na sehemu kubwa ya Serbia, inayokaliwa na Waserbia hasa, wakazi wengi wa Kosovo ni Waalbania waliokuwa takriban robo tatu ya watu wote wa Kosovo hadi mwaka 1990.

Ilikuwa na haki za jamhuri ndani ya shirikisho, lakini kutokana na uhusiano wa kihistoria haikupewa hadhi ya jamhuri kamili.

Wakati wa kusambaratika kwa Yugoslavia viongozi wa Serbia walifuta hali ya kujitawala ya Kosovo na kuwaachisha kazi maofisa wengi wenye utamaduni wa Kialbania.

Hii ilisababisha kipindi cha upinzani na ghasia ndani ya Kosovo kwa haki za Waalbania zilizokandamizwa na polisi na jeshi la Serbia.

Mwaka 1996 vikundi kadhaa vya Kialbania vilianza kuchukua silaha na kupigania uhuru kwa njia ya kijeshi na jeshi la Serbia likajibu vikali na raia kadhaa waliuawa.

Mwaka 1999 wakimbizi wengi kutoka Kosovo walitafuta kimbilio katika nchi jirani na Umoja wa Ulaya.

Baada ya majadiliano juu ya usuluhisho kushindikana, Jeshi la Kujihami la Amerika Kaskazini (NATO) liliamua kuingilia kati kwa kusudi la kuzuia kuongezeka kwa wakimbizi na mauaji.

Machi 24, mwaka 1999 ndege za kivita zilianza kushambulia madaraja, barabara, vituo vya umeme na taasisi za kijeshi katika Serbia.

Jeshi la Serbia likaongeza kampeni yake katika Kosovo na idadi ya wakimbizi ikaongezeka tena.

Mbali na hayo Kosovo ni mwanachama wa Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). **MITANDAO**



# Wataka kasi maboresho Sheria ya Ndoa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeobwa kuharakisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ili kusaidia kuondoa tatizo la ndoa za utotoni pamoja na mimba katika umri mdogo linaloendelea kushamiri.

Ombi hilo lilitolewa juzi na wadau wa masuala ya kulinda haki za watoto katika semina na kamati za kudumu za Bunge za Katiba na Sheria pamoja na ile ya Maendeleo ya jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi, alisema kuwa sheria hiyo inatakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuendana na wakati uliopo sasa.

Alisema, eneo ambalo wanalipigia kelele katika sheria hiyo ya ndoa ya mwaka 1971, ni kifungu cha 13 na kile cha 17 ambavyo vinaruhusu mtoto wa kike mwenye umri wa kuanzia miaka 14, kuolewa kama wazazi wake wataridhia.

"Sheria hii inatoa mwanya kwa wazazi kuitumia kuwalinda waharifu ambao wamekuwa wakijihusisha na matukio ya kuwapa mimba watoto chini ya umri wa miaka 18, hasa katika vifungu hivi viwili unakuta mtu anampa mimba mwanafunzi lakini wanajamii wanamshauri amuoe ili kama watu wataenda mahakamani basi atatambulika kama mke wake kupitia kifungu namaba 13 na 17 cha sheria ya ndoa ya mwaka 1971," alisema Gyumi.

Pia, alisema wadau wanapinga masuala ya ndoa katika umri mdogo, hivyo wanaiomba serikali ifanye marekebisho ili umri wa mtoto kuolewa uwe kuanzia miaka 18, ili kuondoa upungufu ulipo sasa.

Aidha, alisema kuwa mtoto kuolewa chini ya miaka 18, kuna madhara makubwa kuliko faida zilizopo.

Alisema, mtoto kuolewa katika umri huo ambao unaelekezwa katika sheria hiyo unamyima haki zake za msingi ikiwamo kusoma.

"Mtoto huyo katika umri huu wa miaka 14 hadi 16 ni umri mdogo sana kwakua anakuwa bado hajakoma kiakili, kimwili hata kisaikolojia, hata katika ufanyaji wa uamuzi sahihi, hivyo tunao wajibu wa kuweka sheria ambayo itawalinda mabinti zetu katika umri huu"alisema

Gyumi, alisema kuwa Tanzania inashika nafasi ya 11, kidunia kwa mataifa ambayo yana matukio mengi ya ndoa katika umri mdogo.

Alisema pia madhara mengine kwa watoto kuolewa katika umri huo ni pamoja na kuathirika kisaikolojia, magonjwa kama vile fistula na vifo wakati wa kujifungua kutokana na miili yao kutokuwa tayari kwa ajili ya kujifungua.

"Serikali inatumia kiasi kikubwa cha fedha kwajili ya kutibu magonjwa kama fistula ambayo yamekuwa wakiwayapata watoto wengi baada ya kujifungua katika umri mdogo kama sheria itasema ni kuanzia miaka 18 ndiyo umri wa kuolewa basi tatizo hili litapungua," alisema.

Naye Wakili kutoka shirika hilo la msichana Initiative, Jebra Kambole, alisema kuwa moja ya upungufu katika sheria hiyo ni kuwa inampa mtoto haki ya kuolewa lakini haimpi haki zingine.

"Katika sheria hii mtoto wa umri wa kuanzia miaka 14 anayo haki ya kuolewa lakini kama ndoa imemshinda hana haki ya kufungua shauri mahakamani kutaka kutoka kwenye ndoa kwani sheria inamruhusu mtu mwenye umri wa kuanzia miaka 18 tu kufungua shauri"alisema Kambole

Alisema ni vizuri sheria ikaweka umri wa miaka 18, kwani ndicho kipindi ambacho mtoto angalau anakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi sahihi na kuwa tayari kimwili na kifikra.

Alisema, suala la kufanya marekebisho ya sheria hiyo ni agizo la Mahakama kwa serikali ambapo ilitaka kupitia mwanasheria mkuu wa serikali kupeleka muswada wa marekebisho hayo bungeni.

Makamu Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Bunge, Staslaus Nyongo, alisema ni wakati muafa sasa kufanyiwa marekebisho ya sheria hiyo.

"Wenzetu hawa wamefanya tafiti mbalimbali lakini na sisi kama bunge tunao wajibu sasa wa kuona umuhimu wa kufanyia marekebisho ili kuwalinda watoto wetu wa kike kwa umoja wao na adha ambazo wamekuwa wakizipata sasa, alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Serera, akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha kujenga uelewa kwa viongozi, watendaji na wawezeshaji kuhusu utekelezaji wa kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya mpango wa kunusuru kaya maskini wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wilayani humo mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mil. 270/- kusambaza mifumo majitaka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa Mtaa wa Kinyambwa Road, jijini Dodoma, wamepitisha mradi wa Sh. milioni 270.5 kwa ajili ya kusambaza mifumo ya majitaka katika eneo hilo ili kuondokana na adha ya kusambaa mitaani kwa maji taka kila msimu wa mvua.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Lukanus Kayombo, akizungumza na wakazi wa mtaa huo katika mkutano wa hadhara, alisema mradi huo ni muhimu ili kuwasaidia wananchi hao kuondokana na adha ya maji taka.

Alisema wakati wa msimu wa mvua wananchi wamekuwa wakipata adha kutokana na makaro mengi ya vyoo kujaa kutokana maji ya mvua.

"Wakati wa mvua watu wanapata adha sana kwani watu wanalazimika kila wakati kukodi magari kwa ajili ya kunyonya majitaka kutokana na makaro kujaa kila mara kwa mara"alisema Kayombo

Alisema kuwa mradi huo kama utakamilika utasaidia kuondoa adha hiyo kwa wakazi hao hasa wakati wa mvua za masika."Hivi sasa wakati wa mvua mtu ananyonya maji taka zaidi ya mara nne na kiasi cha fedha kinachotumika ni kikubwa sana, hivyo basi mradi huu utakuwa mkombozi kwetu sisi kwani tukiufanya kwa pamoja tutaweza kupunguza gharama za uunganishaji huduma hii kila kaya," alisema.

Aidha, alisema katika mradi huo wananchi watalazimika kila kaya kuchangia fedha, walichokubaliana na kiasi kingine Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Dodoma (DUWASA)watachangia.

"Kama tutakubaliana na huu mradi Duwasa wametuahidi kuchangia mabomba yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 60.5," alisema Kayombo.

Katibu wa kamati ya mradi huo, Peter Ishebabi, alisema wameshaandaa mchoro kwa kushirikiana na wataalamu na kinachosubiriwa ni wananchi kukubaliana ili kuanza kuchangia fedha kwa ajili ya ujenzi.

"Mradi huu kwa namna tulivyo utayarisha utasaidia kupunguza gharama za mtu mmoja mmoja kuunganisha huduma hii kwani bomba pamoja na chemba zitapita kila eneo la makazi ya wananchi," alisema.Hata hivyo, alisema kuwa pamoja na kuondoa adha kwa wakazi hao, pia mradi huo utasaidia kulinda mazingira pamoja na kuondokana na magonjwa ya mlipuko.

# DC ataka uaminifu uhakiki kaya maskini

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Serera, amewataka wawezeshaji wa sehemu ya pili ya mradi wa kaya masikini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) awamu ya tatu kuwa uaminifu katika kusimamia uhakiki upya wa kaya hizo.

Dk. Serera alitoa kauli hiyo jana wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha kujenga uelewa kwa viongozi, Watendaji ,Wakuu wa idara na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo pamoja na wawezeshaji kuhusu utekelezaji wa sehemu ya pili ya TASAF awamu ya tatu.

Aliwataka wawezeshaji hao wa utekelezaji wa mradi huo sehemu ya pili ya awamu ya tatu kuwa waaminifu katika kuhakiki na kuzibaini kaya maskini.

"Utekelezaji wa mradi huu ukafanyike kwa uaminifu wa hali ya juu, bahati nzuri kwenye wilaya yetu, makundi yote yameshirikishwa, hivyo nendeni wote mkasimie uhakiki wa kaya mpya maskini kwa haki "alisema

Aidha Dk. Serera aliwataka wataalamu wa halmashauri hiyo kuwasaidia wanachi katika utekelezaji wa mradi huo kwa kutoa maelekezo ya kitaalamu kwenye maeneo husika.

Alisema kuna baadhi ya kaya hizo maskini nchini wamekuwa wakishindwa kujikwamua kwenye lindi la umaskini kwa kukosa wataalamu wa kuwashauri namna ya kutumia fedha za ruzuku.

Ofisa Ufuatiliaji TASAF Wilaya ya Kongwa, Sopi Samwel, alisema kikao kazi hicho kinashirikisha watu zaidi ya 30 kutoka halmashauri hiyo.

Alibainisha washiriki hao ni madiwani, Kamati ya Ulinzi na Usalama Wakuu wa Idara na wawezeshaji wa utekelezaji wa mradi huo kutoka halmashuari hiyo wote wamepata mafunzo namna ya kushiriki kwenye uhakiki huo.

Alibainisha kuwa TASAF imekuwa ikitoa ruzuku kwa walengwa 7,354 kwa vijiji 51 vya halmashauri hiyo tangu kuanzishwa . Pia alisema katika utekelezaji wa sehemu ya pili ya TASAF awamu ya tatu jumla ya vijiji 36 ambavyo havikuwapo kwenye mradi vinatarajia kuingizwa na kufikia vijiji 87 kwa wilaya nzima.Aidha, alisema uhakiki huo na utambuzi utafanyika upya kwa vijiji vyote pamoja na kuwabaini waliokosa sifa za kuendelea kupata ruzuku ya serikali kupitia mradi huo.

Mtaalamu wa ufuatiliaji na tathimini TASAF makao makuu, Fariji Mishael, aliyemwakilisha Mkurungenzi Mkuu, Tasaf, Ladislaus Mwamanga, alisema mpango huo umeonyesha kupungua kwa hali ya umaskini kwa asilimia 10.

Aliongeza kuwa kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF kitatekelezwa katika halimashauri zote 184 za Tanzania Bara naWilaya zote za Zanzibar.

Alibainisha kuwa utekelezaji huo utafanyika kwenye mitaa, vijiji na shehia zote nchini na kujumuisha maeneo ambayo hayakupata fursa hiyo katika kipindi cha kwanza ambacho kimekamilika .Mishael alisema kipindi cha awamu ya tatu yaTASAF kitafikia kaya 1450,000 zenye jumla ya watu milioni saba nchini hii ikiwa ni ongezeko la kaya 350,000.



## Wafugaji wajengewa uwezo malisho bora

**Na Ashton Balaigwa,** RUNGWE

SERIKALI inakusudia kuwajengea uwezo wafugaji ili kujua uendelezaji wa malisho bora katika maeneo mbalimbali nchini ambayo yatawahakikishia kuwa na mifugo yenye afya bora na kuongeza kipato cha kaya.

Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ugani wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angelo Mwilawa, alisema hayo juzi wakati akizungumza katika mafunzo ya uendelezaji wa malisho yaliyofanyika katika wilayani hapa.

Dk. Mwilawa alisema hatua hiyo ya kuwaendeleza wafugaji ni maagizo ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ili kutoa elimu ya kutosha kwa wafugaji kufuga kisasa.

Akizungumzia malisho ya nyasi aina ya Brachiaria ambazo zimefanyiwa utafiti na watafiti kutoka mradi wa Innove Africa ulio chini ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Dk. Mwilawa alisema una mafanikio makubwa ambao utawasaidia wafugaji.

Mkurugenzi huyo aliwataka wafugaji wa wilaya hiyo na kote nchini kuhakikisha wanaendeleza teknolojia hiyo kwa kupanda na kustawisha nyasi ili kupata uwakika wa chakula cha mifugo yao.

"Wafugaji kote nchini changamkieni hii aina ya malisho ya Brachiaria ni moja ya aina ya nyasi ambazo zimefanyiwa utafiti nchini na ina ubora mkubwa katika kuleta lishe bora kwa mifugo," alisema.

Mmoja wa watafiti katika mradi huo, Dk. Ismail Suleiman, alisema teknolojia hiyo imepokewa vizuri na wafugaji wengi wilayani Rungwe na kuanza kuzipanda nyasi hizo baada ya kubaini zinasaidia uhakika wa chakula cha mifugo katika kipindi chote na kuepusha migogoro baina yao na wakulima.

Alisema mradi ulianza na wafugaji wachache lakini kwa sasa idadi imekuwa ikiongezeka siku hadi siku na kwamba baadhi waliamua kupanda malisho hayo wakati wa kiangazi na kumwagilia kwa maji ili kuhakikisha wanakuwa na malisho muda wote.

Mmoja wa wanufaika hao, Anyabwile Mwakosya, ambaye aliamua kupanda wakati wa kiangazi, alisema awali alikuwa akichukua nyasi porini na zilikuwa zikisababisha madhara kwa mifugo yake lakini kwa sasa tatizo hilo halipo.

Akifungua mafunzo hayo ya siku moja, Mkurugenzi wa Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalam, Prof. Esron Karimuribo, alisema SUA inajivunia kuwa mshiriki katika miradi mbalimbali ya maendeleo inayoboresha maisha ya watu.

# Shule iliyojengwa mwaka 1946 taabani

**Na Grace Mwakalinga,** LUDEWA

ZAIDI ya wanafunzi 300 wa Shule ya Msingi Manga, iliyoko Ludewa mkoani Njombe, wanashindwa kuendelea na masomo kila mvua inaponyesha kutokana mapaa ya majengo kuvuja kutokana na uchakavu.

Shule ya Msingi Manga ilijengwa mwaka 1943 na tangu wakati huo imekuwa ikitumika bila kufanyiwa ukarabati, sasa imechakaa kiasi cha kusababisha mazingira ya utoaji wa elimu katika kuwa magumu.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Odeta Mganwa, alisema kuna madarasa manane yanayotumika kwa wanafunzi kuanzia darasa la awali hadi la saba.

Alisema hali ya miundombinu shuleni hapo hairidhishi kwa sababu madarasa ni mabovu, mbao za makenchi zimeoza, hivyo kuhatarisha usalama wa wanafunzi na madirisha hayotoi hewa ya kutosha.

Diwani wa Kata ya Madilu, Eugen Mlwilo, alisema jengo jipya lililoko shuleni hapo lilijengwa mwaka 1989.

"Hali ya miundombinu ya shule yetu hairidhishi kabisa. Hii shule ina miaka 79 tangu kuanzishwa kwake lakini miundombinu ya majengo hairidhishi. Nimekuwa nikifuatilia Halmashauri ya Ludewa kujua hatma ya kuboresha lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika," alisema Mlwilo.

Kilio cha uchakavu wa shule hiyo kimeanza kuwafikia wadau wa elimu ikiwamo benki ya NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo imeguswa na kero hiyo

Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Straton Chilongola, alisema elimu na afya ni nguzo muhimu, hivyo kwa kutambua kazi zinazofanywa na serikali kuboresha sekta hizo, waliamua kuchangia ujenzi wa shule hiyo.

Akipokea msaada wa mabati 200 ambayo yalitolewa na Benki ya NMB, Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Andrew Tsere, alisema shule yote inahitaji ukarabati na kutoa maelekezo kwa wananchi kujitoa nguvu kazi ili kuanza ujenzi.

Alisema wananchi wa Kijiji cha Manga si maskini kutokana na shughuli za kilimo wanazozifanya kikiwemo kilimo cha viazi na miti, hivyo wakiamua kuchangishana fedha watajenga shule hiyo huku serikali nayo ikiweka mkono wake baada ya kuona jitihada za wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Reuben Mfune, akifungua mkutano wa uchaguzi wa Baraza la wazee la Wilaya hiyo, mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki, ambapo walichagua Mwenyekiti, Makamu, Katibu na Mtunza hazina ili kutetea na kuwasilisha kero zinazowakabili kwenye ngazi za uamuzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TMDA yateketeza shehena ya dawa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imekamata na kuteketeza dawa za binadamu na mifugo ambazo zilikutwa na dosari mbalimbali.

Miongoni mwa dosari hizo ni kutokusajiliwa na zingine kuisha muda wa matumizi huku zikiendelea kutolewa kwenye maduka na vituo vya afya.

KAIMU Meneja wa TMDA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Anitha Mshigati, aliyasema hayo juzi wakati wa kuteketeza dawa hizo katika Mji wa Mbalizi nje kidogo ya jiji la Mbeya.

Alisema uchomaji wa dawa na vifaa tiba ni matokeo ya msako mkali walioufanya kwenye maeneo mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kubaini uingizwaji kinyemela wa dawa ambazo hazijasajiliwa na zingine kumalizika muda wa matumizi huku zikiendelea kuuzwa kwenye baadhi ya vituo vya afya na maduka ya dawa

"TMDA tumekuwa tukifanya ukaguzi kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye mipaka ya nchi na maeneo mengine ya kutolea huduma za afya.

Tumefanikiwa kukamata baadhi ya dawa zilizokwisha muda wake lakini zikiendelea kutumiwa. "Moja ya majukumu yetu tukibaini dawa zinazotumika ama zimekwisha muda wake au hazijasajiliwa, tunazichukua na kufanya mahojiano ya kina ili kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria ikiwamo kutozwa faini na kulipa ada ya kuteketeza bidhaa hizo," alisema Mshigati.

Alisema hadi sasa waliobainika kufanya vitendo hivyo walichukuliwa hatua ya kulipa faini ya kukutwa na bidhaa hizo lakini pia kulipa ada ya kutekeleza vifaa tiba na dawa zilizokamatwa.

TMDA, alisema inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kutambua bidhaa zinazotakiwa kwa ajili ya matumizi kwa kuhakikisha wanahakiki muda wa matumizi na ubora wa bidhaa yenyewe kabla ya matumizi.

Alisema madhara ya kutumia bidhaa duni ni makubwa Kwa afya ya mwanadamu hivyo kuwasihi kutokubali kununua au kuuza bidhaa yenye gharama nafuu badala yake wazingatie ubora na usalama wa bidhaa yenyewe kwa kufanya ukaguzi kabla ya kutumia.

Meneja huyo alisema oparesheni ya kukagua ubora na usalama wa dawa na vifaa tiba ni endelevu kwa kuhakikisha wanaondoka katika soko kwa kuviteketeza ili kulinda afya za wananchi.

Baadhi ya wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, walipongeza TMDA kwa kutekeleza bidhaa hizo na kwamba elimu inahitajika zaidi kwa jamii ili kutambua ubora na usalama wa bidhaa kabla na baada ya kuzitumia.

Mmoja wa wananchi hao, Bupe Amos, alisema wanawake ni waathirika wakubwa wa matumizi wa bidhaa feki au zilizokwisha muda hususani mafuta na kwamba wanashawishika kununua bidhaa hizo kutokana na unafuu wa bei lakini pia tamaa ya kung'arisha rangi zao ili kuongeza mvuto.



## Waziri akerwa utoro shuleni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amewataka walimu wa Shule ya Kisiwa Panza Kisiwani Pemba kushirikiana na wazazi kutatua changamoto ya utoro inayoikabili shule hiyo.

Aliyasema hayo jana katika ukumbi wa kituo cha ubunifu wa Kisayansi Kisiwa Panza wakati akizungumza na walimu, watendaji wa kituo na kamati ya shule hiyo alipofanya ziara ya kuitembelea shule hiyo.

Waziri Simai alisema utoro ni miongoni mwa sababu zinazopelekea kushuka kwa ufaulu katika shule hiyo, hivyo aliwaomba walimu kubuni mbinu shirikishi zitakazosaidia kukabiliana na tatizo hilo.

Aidha, aliwataka walimu kuongeza kasi na ari ya ufundishaji sambamba na ubunifu ili kuwajengea hamu na ari wanafunzi ya kupenda kujifunza.

Naye Ofisa Mdhamini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Moh'd Nassor Salim, aliwataka watendaji wa kituo cha ubunifu wa kisayansi kuhakikisha wanaweka vipindi vya kufundisha katika shule hiyo.

Alisema haikubaliki kuona wanafunzi wa Shule ya Kisiwa Panza wanakosa mwalimu kwa baadhi ya masomo wakati katika kituo cha ubunifu wapo walimu wa masomo mbalimbali.

Kwa upande wao wazazi wa wanafunzi wa shule hiyo, walieleza matatizo mbalimbali yanayoikabili shule ukiwamo uhaba wa vyumba vya kusomea na uhaba vyoo, hali ambayo hupelekea wananfunzi kupata maradhi mbalimbali ikiwamo UTI.

Khamis Juma Othman, mjumbe wa kamati ya shule hiyo, aliiomba wizara kukamilisha ujenzi wa vyumba viwili vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi ili kusaidia kupunguza tatizo hilo.

**Aidha, aliwataka walimu kuongeza kasi na ari ya ufundishaji sambamba na ubunifu ili kuwajengea hamu na ari wanafunzi ya kupenda kujifunza.**

# SMZ yalihakikishia ushirikiano kanisa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeuhakikishia uongozi wa Kanisa la Waadventista Wasabato Tanzania kwamba itaendelea kushirikiana nao na inatambua mchango wao katika kusaidia huduma za jamii Zanzibar.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo juzi Ikulu Jijini Zanzibar alipokutana na uongozi wa kanisa hilo.

Dk. Mwinyi alisema kwamba Serikali anayoiongoza itaendeleza ushirikiano wake kwa Kanisa hilo kutokana na kuthamini mchango wake mkubwa katika kutoa huduma za jamii.

Alisema kuwa kanisa hilo limewajenga kiimani waumini wake katika kushirikiana na Serikali katika kuimarisha sekta ya elimu pamoja na sekta ya afya kwa Unguja na Pemba.

Alieleza kuwa juhudi za Kanisa hilo za kusaidia katika sekta ya afya na sekta ya elimu zitaendelea kuungwa mkono ikiwa ni pamoja na kuhakikisha inazifanyia kazi changamoto zilizopo.

Alieleza kuwa Serikali itakuwa tayari katika kuhakikisha miradi inayoanzishwa na Kanisa hilo ikiwemo ya elimu na afya inafikia malengo yaliyokusudiwa katika kutoa huduma kwa jamii.

Aidha, alitoa pongeza kwa Kanisa hilo kwa kusaidia katika kuunga mkono juhudi za Serikali kwenye sekta ya elimu kwa kusaidia uimarishaji wa sekta hiyo katika Shule ya Ali Khamis Camp iliyopo Pemba kwa kusaidia walimu wa Sayansi pamoja na vitabu.

Pia, alilipongeza Kanisa hilo kwa kusaidia uimarishaji wa sekta ya afya katika zahanati yake iliyopo Meya katika eneo la Magomeni Zanzibar ambayo ikitoa huduma za afya kwa kipindi kirefu.

Rais Dk. Mwinyi aliupongeza utayari wa Kanisa hilo wa kutaka kuanzisha chuo cha ufundi, hatua ambayo itasaidia kuimarisha sekta ya elimu na ufundi hasa kwa vijana.

Naye Askofu Mark Malwa Malekana ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Kanisa la Waadventista wa Sabato Tanzania na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Kusini mwa Tanzania, akiwa na ujumbe wake wa Maaskofu kutoka Zanzibar na Tanzania Bara, walimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kasi kubwa ya kuiletea maendeleo Zanzibar aliyoanza nayo ikiwa ni pamoja na maono yake ya uchumi wa bluu huku akiahidi kwamba Kanisa lake litaendelea kuiunga mkono Serikali katika kufikia malengo yake iliyojiwekea.

Akitoa historia ya Kanisa hilo Askofu Malekana alisema kuwa kwa Zanzibar Kanisa hilo lilianza mwaka 1986 ambapo kuanzishwa kwake kuliambatana na utoaji wa huduma za kiroho na za kijamii.

Alisema kuwa katika huduma za kijamii, Kanisa hilo lilianzisha huduma za utabibu kwa kuwa na vituo viwili vya afya Unguja na Pemba pamoja na kuanzisha Shule ya maandalizi na msingi huko Tomondo na kwa sasa limo katika hatua ya kuanzisha Shule ya Sekondari.

Alisema kuwa elimu inayotolewa na shule zao inazingatia mitaala na miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu pamoja na kutoa elimu bila ya kujali tofauti za kidini au kikabila.

Kwa upande wa Pemba alisema kwamba Kanisa hilo lilitoa vitabu katika Shule ya Ali Khamis Camp vyenye thamani ya Sh.milioni nne pamoja na kutuma walimu wawili wa masomo ya Sayansi ambao walikuwa wakihudumiwa na Kanisa kwa miaka mitano mfululizo hatua iliyopelekea kuongeza ufaulu katika shule hiyo.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, akikagua madaftari ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kisiwa Panza, alipofanya ziara ya kikazi shuleni hapo, Kisiwani Pemba jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tani za mchele mbovu zateketezwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKALA wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA) imeteketeza tani za mchele mbovu ambao haufai kwa matumizi ya binadamu.

Mchele huo aina mapembe chereko ambao ni maarufu Visiwani Zanzibar, umeteketezwa katika dampo la Mkoa wa Kusini Unguja.

Akizungumza jana baada ya uteketezaji huo, Mkuu wa Usajili na Tathmini ya Chakula kutoka ZFDA, Khadija Ali Shekha, alisema mchele huo umeingizwa nchini na kampuni ya Zenji General Mechandiser inayomilikiwa na mfanyabiashara Salum Turki.

Alieleza kuwa mchele huo uliingizwa nchini Desemba mwaka jana ukitokea nchini India ambako ulikuwa upo sokoni.

Aidha, alisema kuwa mchele huo uligundulika kutofaa kwa matumizi ya binadamu kutokana na harufu mbaya, kujaa wadudu na mavumbi ambapo ungeendelea kutumiwa ungesababisha madhara makubwa ya kiafya kwa mtumiaji.

Alisema ni vyema wafanyabiashara kuwa makini wanapoleta bidhaa zao nchini ili kuepuka hasara inazoweza kujitokeza ikiwamo kupata hasara ya kuteketezwa kwa bidhaa hizo.

"Sisi bodi tumekuwa tunaangamiza bidhaa hizi kwa kushirikiana na kwa karibu na gharama wamekuwa wakitoa wenyewe hivyo, tujitahidini tulete bidhaa zilizokuwa bora," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wafanyabiashara kuacha kuagiza bidhaa zao kupitia mitandao ya kijamii ili kuepusha hasara ikwao.

Naye, Ofisa Mazingira kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, Muhsini Ali, alisema, wamekuwa wakisimamia uteketezaji huo ili zoezi hilo kufanyika bila ya kuathiri mazingira.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**KatikaMahakamayamwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamiziwamirathi**
**NO.94/2021**

Ombi la **CATHERINE JOSEPH MLOKA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **JOSEPH MORIS MLOKA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **13/05/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 08/04/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GAGI

**DANGANA OMOTOKE BLESSING** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA EXTRAIL** yenye namba za usajili **T 805 BRU** chasisi namba **NT30059119** engine namba **GR20212886A**,yeyote atakayeikota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/URA/RB/181950/2021**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**
**SHAURI NO.173/2020**
**JOSEPHINA MAHENGE::::::::::::::::::::::::MDAI**
**Dhidi ya**
**ORDAN CHAULA:::::::::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**TROPICAL SEED LTD:::::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**NMB BANK PLC:::::::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**YAH : KUITWA SHAURINI**
**KWA :**
**ORDAN CHAULA NA TROPICAL SEED LTD**

Fahamu kwamba JOSEPHINA KORINELI MAHENGE amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 06/05/2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka : Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 13/04/2021.

**A.Mapunda**
**MWENYEKITI**
**13/04/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**KatikaMahakamayamwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamiziwamirathi**
**NO.112/2021**

Ombi la **FRANK FUNGO MWEZI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **IMAKULATA MWEZI FUNGO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **28/04/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe19/04/2021**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**KatikaMahakamayamwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamiziwamirathi**
**NO.113/2021**

Ombi la **JUDICA YESAYA MUNGURE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **YESAYA JOELI MUNGURE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **27/04/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe19/04/2021**

K-FINANCE

## NOTISI

Kampuni ya K-Finance ikishirikiana na Majembe Auction Mart wanatoa notisi ya siku (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa mdaiwa (mkopaji) **SAMWEL ZABDIEL TARIMO (ENERGY FORWARDERS LIMITED)** na Mdhamini wake **RICHARD TARIMO** wanatakiwa kulipa deni lote ndani ya muda uliotolewa. Ikiwa watashindwa kulipa ndani ya muda tajwa dhamana ambayo ni gari litauzwa kwa mnada wa hadhara.

**Kwa maelezo Zaidi wasiliana kwa namba 0715 980025/ 0738 165606/0738 165605.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**KatikaMahakamayamwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamiziwamirathi**
**NO.87/2021**

Ombi la **SHEILA MSAFIRI MAGENI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **HAMISI JACKSON MALIPULA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 06/05/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .


Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe06/04/2021**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ALEX ZAKARIA SIGALA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye Index No. **S.0341/0619.** Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2012 **SANGU SECONDARY.**
Cheti cha kidato cha nne chenye Index No. P 0211/0194. Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2009 **LOLEZA SECONDARY,** Cheti cha elimu ya secondary chenye **Index No. S 0150/0008.** Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2008 **SAME SECONDARY**
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu naye.
Polisi taarifa **IRI/MUF/RB/195923/2021.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALLY ABDALLA MOHAMED** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0509/0089/2015** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **UCHIRA** mwaka **2015**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/KIG/RB/671684/2020**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**KatikaMahakamayamwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamiziwamirathi NO.115/2021**
**Ombi la HAPPY THOMAS CHUMA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu THOMAS SALES NG`ATANGWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 24/04/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe20/04/2021.

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**KatikaMahakamayamwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamiziwamirathi**
**NO.179/2017**

Ombi la **LUBUVA LEONARD MARUSU** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **LEONARD STEPHAN MARUSU**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **22/04/2021 kabla huyo mwombaji** hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 12/04/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BRUNO ALBIN KIMARO** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 667 DTW TOYOTA IST.** Chassis namba **NCP600148649.** Engine namba **2NZ3065905.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DAR/URA/RB/203164/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VICTOR RWEYONGEZA RUGAIKA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 379 CCF TOYOTA NOAH.** Chassis namba **AZR600050085.** Engine namba **1AZ418868.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DAR/URA/RB/203743/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**KatikaMahakamayamwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamiziwamirathi NO.117/2021**
**Ombi la SAIDI KENEDY SAIDI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu HADIJA SAIDI MDENG`O**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 04/05/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe20/04/2021

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Rais Idriss Deby wa Chad auawa

**N'Djamena,** CHAD

RAIS, Idriss Deby wa Chad, ameuawa baada ya kutembelea vikosi vilivyokuwa mstari wa mbele, kikipambana na kundi la waasi la Front for Alternation and Concord Chad (FACT), Kaskazini mwa nchi.

Shirika la habari la kimataifa la AFP lilimnukuu msemaji wa jeshi kuwa, mtoto wa rais aliyeuawa ndiye atakayeliongoza baraza la kijeshi linaloongoza nchi hiyo kwa sasa.

Mtoto huyo, Mahamat Idriss Deby ni manajeshi wa cheo cha juu cha jenerali ambaye mwaka jana, alipewa cheo cha juu zaidi cha kijeshi cha 'Field Marshall' kutokana na harakati zake.

Serikali na bunge limevunjwa na sasa baraza la kijeshi ndilo litakaloiongoza nchi hiyo kwa kipindi cha miezi 18 ijayo.

Jeshi limetangaza marufuku ya kutoka nje wakati wa usiku, kuanzia saa 12 jioni mpaka saa 11 alfajiri kuanzia jana, huku mipaka yote ya nchi na anga ikifungwa.

Kifo chake kinatokea baada ya saa chache kutangazwa kushinda kwa kishindo na kuongoza kwa asilimia 80 kwenye uchaguzi wa urais, kulingana na matokeo ya awali yaliyotangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi (CENI).

**Deby mwenye Umri wa miaka 68, amefariki baada ya kushinda uchaguzi kuongoza taifa hilo kwa muhula wa sita katika uchaguzi ambao upinzani ulisusia.**

Uchaguzi wa urais ulifanyika Aprili 11, mwaka huu na CENI kumtangaza Rais Deby (68) kushinda kwa kura nyingi karibu katika maeneo yote, isipokuwa eneo moja kati ya 51.

Kilmapone Larme, anayehusika na masuala ya vifaa katika CENI, alisema bado hawajapata zaidi ya asilimia 30 ya matokeo ya uchaguzi.

Kundi la waasi lenye makao yake nchini Libya, Front for Alternation and Concord in Chad (FACT), lilishambulia kituo vikosi vya Chad kwenye mpaka wa nchi hiyo Kaskazini mwa nchi, siku ya uchaguzi, huku upinzani ukisusia uchaguzi huo.

Msemaji wa Jeshi, Azem Bermendao Agouna alitangaza kifo cha Rais Deby, kupitia televisheni ya serikali huku akiwa amezungukwa na kundi la maofisa wa jeshi akitaja kama Baraza la Taifa la Serikali ya Mpito.

Rais Deby, amekuwa madarakani tangu mwaka 1990 baada ya mapinduzi ya kijeshi na kuwa kati ya



viongozi wa Afrika waliodumu madarakani kwa muda mrefu na ushindi wake uliotangazwa Aprili 18, mwaka huu, ungekuwa wa awamu ya sita. Sababu ya kifo chake hazikutajwa wazi.

"Wito wa mazungumzo ya amani umeanza kwa Wanachad wote nchini na nje, ili kuendelea kijenga nchi pamoja," alisema msemaji huyo.

"Baraza la Mpito la Taifa linawahakikishieni Wanachad kwamba hatua zimechukuliwa kuhakikisha amani, usalama upo. Amefariki akipigania usalama wa taifa letu,""

Jeshi la Chad lilieleza zaidi kuwa Rais Deby, alifariki baada ya kupata majeraha kwenye mapambano dhidi ya waasi, ambao walifanya mashambulizi wakijaribu kuteka mji mkuu, N'Djamena.

Rais wa Chad Idriss Deby, ambaye amekuwa madarkani kwa muda wa miaka 30, amefariki mapema leo kutokana na majeraha aliyopata wakati wakiongoza wanajeshi wake kupambana na wanajihadi kaskazini mwa taifa hilo, taarifa kutoka kwa jeshi imesema.

Kupitia taarifa ya msemaji wa jeshi, Jenerali Azem Bermandoa Agouna amesema

Deby mwenye Umri wa miaka 68, amefariki baada ya kushinda uchaguzi kuongoza taifa hilo kwa mhula wa sita katika uchaguzi ambao upinzani ulisusia.

Deby amekuwa miongoni mwa marais wa muda mrefu barani Afrika baada ya kuchukuwa hatamu za uongozi mwaka 1990, kupitia njia ya mapinduzi. Vikosi vya jeshi vya Chad, vimekuwa vikikabiliana kwa wiki moja na kundi la waasi la FACT, baada ya kupingia kupitia Kaskazini mwa nchi kutoka ngome kuu nchini Libya.

Kulingana na duru za kuaminika, mapigano yaliendelea hadi mwishoni mwa wiki, hadi juzi. Inasemekana mapigano hayo yalitokea karibu na mji wa Nokou, kilomita 50 kutoka mji wa Mao, mji mkuu wa mkoa wa Kanem.

Mkoa wa Kanem upo katikati mwa magharibi mwa Chad na unaendelea kwenye mpaka na Niger.

Kiongozi wa FACT alibainisha kwamba, idadi kubwa ya wapiganaji wake imetumwa Kaskazini mwa nchi, bila kutoa maelezo zaidi.

Alisema wanafikiria juu ya hatua watakazo chukua katika siku za hivi karibuni, huku akiishtumu Ufaransa kumsaidia Idriss Deby katika mapigano hayo hasa kwa kumpa taarifa za kijasusi, baada ya ndege za Ufaransa kuendelea kufanya operesheni za kijasusi karibu na maeneo wanayoshikilia.

Mwishoni mwa wiki, jeshi hilo lililiambia Shirika la Habari la Reuters, kuwa waasi 300 waliuawa na wengine 150 kukamatwa katika mapambano hayo, huku likipoteza wanajeshi watano na wengine 36 wakijeruhiwa **REUTERS/BBC/RFI**

## Urusi yamtibu mkosoaji wa Putin

**Moscow,** URUSI

KIONGOZI wa upinzaji wa Urusi, Alexei Navalny, amehamishiwa hospitali ya gereza, kwa ajili ya matibabu.

Taarifa kutoka mamlaka rasmi, zilieleza kuwa hali yake kiafya inaridhisha.

Navalny amekuwa kwenye mgomo wa kususia kula chakula kwa siku 20 sasa, akidai anapatiwa matibabu duni.

Hivi sasa mkosoaji huyo, amehamishiwa jiji la Vladimir, umbali wa kilomita 180 (maili 112) Mashariki mwa Moscow.

Mamlaka ya Huduma ya Gereza (FSIN), ilisema Navalny, anachunguzwa na daktari kila siku na amekubali kuchukua vitamin.

Mkosoajia huyo aliwekewa sumu ya kulemaza neva Agosti, mwaka jana na kunusurika kifo.

Baada ya kuhamishiwa hadi kitengo cha wagonjwa mahututi huko Berlin, wataalamu wa sumu walisema sumu hiyo ilikuwa ya kiwango cha silaha ya Urusi, Novichok.

Serikali za Magharibi, ziliilaumu serikali ya Urusi kwa shambulio hilo na Navalny alimlaumu Rais Vladimir Putin, moja kwa moja. **BBC**



Nyumba zikionekana pembezoni mwa udongo uliomeguka katika kijiji cha Nefyn, Wales, Uingereza, juzi na kusababisha baadhi wa wakazi wa eneo hilo kuhamishwa. **PICHA: REUTERS**

## Ujerumani si huru kwa habari

**Paris,** UFARANSA

SHIRIKA la Waandishi wa Habari Wasio na Mipaka (RSF), limeiondoa Ujerumani katika mataifa yanayoongoza kwa uhuru wa habari.

Tathimini mpya ya uhuru wa vyombo vya habari, iliyotolewa na RSF, ilionyesha kati ya mataifa 180 yaliofanyiwa uchunguzi, Ujerumani inashika nafasi ya 13 ikiwa imeporoka kwa nafasi mbili nyuma, ikilinganishwa na mwaka jana.

Msemaji wa RSF, Michael Rediske alisema kushuka huko kumetokana na mashambulizi mengi yaliyofanywa na vyombo vya usalama, wakati wa kukabiliana na ukiukwaji wa masharti ya kukabiliana na virusi vya corona.

Aliongeza kuwa vurugu dhidi ya waandishi habari nchini zimefikia viwango ambavyo havijawahi kutokea.

Mwaka jana, kuliripotiwa visa visivyopungua 65 vya ukandamizaji dhidi ya waandishi habari, ikiwa ni ongezeko la mara tano zaidi ikilinganishwa na mwaka 2019. **DW**

## HABARI MICHEZO



# TUCHEL AMTAKA SULE WA BAYERN

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, ameonekana kutamani kupata saini ya mlinzi wa kati wa Bayern Munich, Niklas Sule, katika jitihada za kuboresha kikosi chake cha msimu ujao, ESPN imeripoti.

Ujio wa Tuchel katika timu ya Chelsea umechangia maendeleo makubwa na kuiwezesha Chelsea kufanya vizuri.

Chelsea chini ya Tuchel imetinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na fainali ya Kombe la FA.

Chelsea watakutana na Real Madrid katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati pia ikikutana na Leicester City katika fainali ya FA Mei 15, mwaka huu.

Kocha huyo wa Chelsea anatumia mfumo wa mabeki watatu wa kati, ambao umeonekana kuwasaidia kwenye kushambulia na kujilinda.

Beki Zouma anaweza akaondoka msimu huu endapo Sule atasajiliwa kutoka Bayern Munich.

Sule amebakiza mkataba wa mwaka mmoja tu pale Munich, na Tuchel anaonekana kumkubali sana beki huyo kisiki wa Bayern.



# *Bayern haina mpango na Super League*

**MUNICH,** Ujerumani

MABINGWA wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich, wameungana na wapinzani wao Borussia Dortmund na RB Leipzig kutangaza kutounga mkono mashindano mapya ya Ulaya.

Klabu 12 kubwa kutoka England, Hispania na Italia zilithibitisha kwamba zinajiandaa kujiunga na mashindano ya Ulaya ambayo yameundwa kwa ajili ya kuleta upinzani kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika taarifa yake Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bayern, Karl-Heinz Rummenigge, alithibitisha kwamba, klabu yake haitashiriki na badala yake watakuwa na mtizamo wa kurekebisha Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"FC Bayern haitashiriki katika mpango wa Super League," alisema Rummenigge.

Wakati klabu zinapotangaza mipango yao ya Super League, UEFA pia ilithibitisha Jumatatu kwamba kutakuwa na Ligi ya Mabingwa iliyorekebishwa kuanzia mwaka 2024.

Muundo mpya utaona timu 36 zinashiriki katika muundo wa ligi moja kuchukua nafasi ya hatua ya makundi.

Kila timu itacheza jumla ya michezo 10 nyumbani na ugenini, na nane bora zitafuzu moja kwa moja kwa 16-bora na zile zinazomaliza kati ya tisa na 24 kushindana katika hatua mbili za kucheza ili kuamua nani mwingine anayeingia hatua ya mtoano.

# Mashindano mapya Ulaya yapingwa kila kona

**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la Vyama vya Soka Ulaya (UEFA), limesema litahakikisha linamfungia mchezaji au klabu yoyote itakayoshiriki kwenye Ligi mpya ya Klabu za Ulaya (European Super League).

Mapema jana Klabu 12 kubwa Ulaya zilitangaza rasmi kuanzisha michuano hiyo kuanzia Agosti hadi Mei mwakani na itafanyika nyumbani na ugenini.

Michuano hiyo itakuwa na jumla ya timu 20 zitazotengeneza makundi mawili, kila moja likiwa na timu 10.

Na watakaomaliza nafasi tatu za juu kila kundi watatinga robo fainali, huku walioshika nafasi ya nne na tano katika makundi yote watapambana kutafuta mshindi mmoja wa kuungana nao robo fainali.

Klabu hizo zilieleza nia yao hiyo na kutaka kuzungumza na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), pamoja na UEFA, lakini taarifa rasmi zinaeleza itafungia timu au klabu yoyote ambayo itashiriki mashindano hayo.

FIFA nao wakaeleza kwamba, kuanzishwa kwa mashindano hayo kutaondoa umoja na mshikamano kwani zitahusishwa timu kubwa tu huku zikiachwa nyingine.

Timu tano kati ya 20 zitakuwa zinashuka kila mwaka na tano kupanda, klabu zilizoridhia kuunda michuano hiyo ni AC Milan, Inter, Juventus, Atletico, Barcelona, Real Madrid, Arsenal, Liverpool, Manchester City, Manchester United, Chelsea na Tottenham Hotspur.

Mashindano hayo yanaonekana kupingwa na watu wengi kutokana na sheria zake na ukweli kwamba zinabagua watu wengine.

Sheria za michuano hiyo zinaeleza kwamba timu 15 zilizoanzishwa hazitashuka daraja, kitu ambacho kocha wa Liverpool Jurgen Klopp anaamini kinapoteza ladha ya mpira.

"Hakuna mtu ambaye anatamani kuona Liverpool vs Real Madrid kwa miaka 16 mfululululizo," alisema Klopp alipoulizwa kuhusu maoni yake.



# Rooney aishangaa Tottenham kumfukuza Mourinho

**LONDON,** England

WAYNE Rooney amesema Tottenham Hotspur ilipaswa kumfanya Jose Mourinho asimamie fainali ya Kombe la EFL, kwani anajua jinsi ya kuunda timu itakayocheza dhidi ya Manchester City.

Siku moja baada ya kuthibitisha kuhusika kwao katika klabu 12 zilizokubali kuungana na Ligi mpya ya Ulaya, Spurs ilitangaza kuondoka kwa Mourinho baada ya kuinoa timu hiyo kwa miezi 18.

Sare ya mabao 2-2 ugenini huko Everton wiki iliyopita ilizidi kuharibu matumaini ya Tottenham ya kumaliza nne bora katika Ligi Kuu England, wakati pia waliondolewa kwenye Ligi ya Europa na Dinamo Zagreb katika hatua ya 16.

Lakini, wana mchezo wa fainali Jumapili hii na watachuana na City huko Wembley, lakini kufukuzwa kwa Mourinho kumeleta mshangao mkubwa kwa Rooney.

"Nadhani ni ujinga kufanya hivyo kabla ya fainali ya kombe, muda wa kushangaza hata hivyo," kocha huyo wa Derby aliwaambia waandishi wa habari.

Rooney alifanya kazi na Mourinho wakati wa msimu wake wa mwisho kama mchezaji wa Manchester United, ikiwa ni pamoja na kuonekana mara chache akitokea benchi kwenye ushindi wa mwisho wa Ligi ya Europa dhidi ya Ajax mwaka 2017.



# NAGELSMANN SASA AIKANA BAYERN



**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann, amesisitiza kuwa hajafanya mazungumzo yoyote na Bayern Munich juu ya kuchukua nafasi ya Hansi Flick pale Allianz Arena.

Flick alitangaza Jumamosi kuwa anatarajia kuondoka Bayern mwishoni mwa msimu, na kocha huyo mwenye umri wa miaka 56, anatajwa kumrithi Joachim Low kama bosi wa Ujerumani baada ya mashindano ya Ulaya.

Uvumi huo ulienea kuwa Nagelsmann tayari amepangwa kuchukua nafasi yake kwa mabingwa hao wa Bundesliga, kitu ambacho kocha huyo mwenye umri wa miaka 33, amekuwa mwepesi kukataa kwa mara ya pili.

Alipoulizwa juu ya mazungumzo ya uvumi na Bayern, Nagelsmann alisema: "Kulikuwa na hakukuwa na majadiliano na hakuna ofa.

"Ndio maana sijui matakwa ya Bayern ni nini. Nimesema sitaki kuanzisha vita na waajiri wangu, hiyo bado ni kesi."

# *Klopp: Kiatu kinamfanya Salah kuwa mbinafsi*

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amekiri kwamba nafasi ya kuwania Kiatu cha Dhahabu kwa mara ya tatu katika Ligi Kuu England imemfanya Mohamed Salah kuongeza ubinafsi.

Klopp amesema mshambuliaji huyo wa Misri anaonekana kukitaka kiatu kwa mara nyingine kwa udi na uvumba.

Salah alimaliza msimu wa 2017-18 katika Ligi Kuu akiwa na mabao 32 na kushinda zawadi hiyo na mwaka uliyofuatia alimaliza akiwa na mabao 22 ambapo Sadio Mane na Pierre-Emerick Aubameyang pia walimaliza wakiwa na idadi hiyo, hivyo wote walitwaa Kiatu cha Dhabau msimu wa 2018-19.

Msimu huu Salah anashika nafasi ya pili katika chati ya utupiaji mabao, akiwa amefunga mabao 19 nyuma ya Harry Kane ambaye amecheka na nyavu mara 21 na amesaliwa na michezo saba pekee kukamilisha msimu.

Klopp alipoulizwa baada ya mchezo dhidi ya Leeds United Jumatatu uliomalizwa kwa sare ya bao 1-1, kama Kiatu cha Dhahabu ndiyo kipaumbele kwa Salah alijibu: "Ndiyo, ni kweli.

"Wachezaji wengi hawajawahi kushinda kiatu hicho kama ukishinda kwa mara ya kwanza ni mafanikio makubwa.

"Kama ukishinda kwa mara ya pili ni mafaniko makubwa zaidi, kama ukishinda kwa mara ya tatu ni nzuri sababu siyo wachezaji wengi walishinda mara tatu kiatu hicho.



# DON… ZA SOKA
## MAG… YA ULAYA




# PEREZ: LAZIMA HAALAND, MBAPPE WATUE MADRID

●●● Mashabiki mara zote wananitaka mimi kumnunua, jibu langu nawaambia msihofu, ukweli ni…

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez, amesema anafanya kila liwezekanalo kwa miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kutopoteza nafasi ya kuwasajili nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe na straika wa Borussia Dortmund, Erling Haaland.

**Madrid imekuwa ikihusishwa sana na mkali wa PSG, Mbappe, huku straika anayewindwa zaidi wa Dortmund, Haaland naye akiwa kwenye rada za Madrid.**

Wakati akijadili kuhusu Ligi mpya ya Ulaya ambapo yeye ni mwenyekiti, Perez alielezea kuhusu uvumi wa Mbappe na Haaland.

"Mashabiki mara zote wananitaka mimi kumnunua Mbappe," alisema Perez akiiambia El Chiringuito.

"Jibu langu? Nawaambia: Msihofu... Ukweli ni kwamba yeye ni mchezaji mzuri, ndio.

"Sijawahi kuzungumzia kuhusu Mbappe. Angalau sasa... Sijui nini kitatokea kuhusu mkataba wake pale PSG."

Kuhusu Haaland, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Barcelona, Manchester City, Manchester United, PSG, Chelsea, Liverpool na Juventus, Perez aliongeza: "Baba yake Haaland alitutembelea kwenye viwanja vya mazoezi pale Valdebebas, ndio.

"Kila mmoja hapa mara zote amekuwa na mawazo hayo, kwamba wanataka kuona wachezaji bora wakubwa hapa.

"Haaland na Mbappe ni wachezaji wawili bora sana, lakini (Lionel) Messi na (Cristiano) Ronaldo walifanya vitu ambavyo ni ngumu kuamini."

Hata hivyo, Perez, alikanusha taarifa kwamba kuna uwezekano wa kuungana na mfungaji wao wa wakati wote klabu hapo, Cristiano Ronaldo. Ronaldo ambaye aliondoka Madrid kwenda Juventus mwaka 2018, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Turin na 'Los Blancos' hao ndio wamekuwa wakihusishwa zaidi na mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or.

Lakini Perez alisema: "Cristiano Ronaldo hatakuja tena Real Madrid.

"Haileti maana, ana mkataba na Juventus. Nampenda sana, ametufanyia mengi hapa."

Perez pia aliulizwa kuhusu majaliwa ya nahodha wa Madrid, Sergio Ramos, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Ramos mwenye umri wa miaka 35, bado hajasaini mkataba mpya pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu na ripoti zinabainisha kwamba, anawaniwa na timu kama Man United, PSG na Chelsea.

"Nampenda Sergio Ramos, lakini tupo kwenye hali mbaya sana ya kifedha hapa Real Madrid," aliongeza Perez, ambaye alisisitiza Vinicius Junior hauzwi.

"Hakuna anayewekeza fedha kwenye klabu hii.

"Ataondoka klabuni? Siwezi kusema hivyo... vitu vingi vinaweza kutokea. Tutafikiria kuhusu hilo mwishoni mwa msimu."

## ZISIKUPITE

### VIEIRA ATAJWA PALACE

NAHODHA wa zamani wa Arsenal, Patrick Vieira, 44, yuko katika orodha ya makocha wanaosakwa na Crystal Palace kama Roy Hodgson, 73, ataondoka mkataba wake utakapomalizika msimu huu wa joto. Mfaransa huyo hana kazi tangu Desemba. ***(Athletic)***

### SPURS WAMTAKA NAGELSMANN

TOTTENHAM Hotspur wanamtaka kocha wa Red Bull Leipzig, Julian Nagelsmann, 33, kuchukua nafasi ya Jose Mourinho, aliyefutwa kazi Jumatatu. ***(Mail)***

### MOURINHO HAKUMTAKA BALE

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, alipinga kusajiliwa tena mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale, 31, kwa mkopo kutoka Real Madrid Septemba. ***(Telegraph)***

### MAITLAND ATAKIWA PALACE

CRYSTAL Palace inawania kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal na England, Ainsley Maitland-Niles, 23. Leeds United na Monaco ya Ufaransa pia zinamfuatilia nyota huyo ambaye yupo West Bromwich Albion kwa mkopo tangu Januari. ***(Mirror)***

### LIVER YAMUWINDA WATKINS

LIVERPOOL wanamtaka mshambuliaji wa Aston Villa na England, Ollie Watkins, 25, ambaye alivunja rekodi ya usajili wa klabu hiyo miezi minane iliyopita alipojiunga nayo kutoka Bretford kwa paundi milioni 28. ***(Football Insider)***

### EN-NESYRI ANUKIA WEST HAM

WEST Ham United wanaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsaini Youssef En-Nesyri kutoka Sevilla, 23, licha ya Liverpool na Manchester United kuhusishwa na mshambuliaji huyo. ***(La Razon)***

### COLEMAN KUWA KOCHA

EVERTON wameanza mazungumzo na mlinzi, Seamus Coleman, 32, kuhusu jukumu la ukocha wakati atakapomaliza muda wake wa kucheza. Mkataba wa Colman kutoka Jamhuri ya Ireland utaendelea hadi Juni mwaka 2022. ***(Liverpool Echo)***

### SULE AWANIWA CHELSEA

CHELSE imeongeza juhudi za kumsaka mlinzi wa Bayern Munich, Niklas Sule, 25, baada ya kocha Thomas Tuchel kutoa kipaumbele kwake. ***(Athletic)***

### BARCA KUMUUZA PUIG

BARCELONA wapo tayari kumwachilia Riqui Puig, 21, aondoke klabuni hapo msimu huu, na wamepokea ofa kutoka klabu za Ligi Kuu England, Italia, Ujerumani na Ureno zinazotaka kumnunua kiungo huyo wa kati wa Hispania. ***(Sport - in Spanish)***

### WARUDI TENA KWA RASHICA

ASTON Villa wanapanga kuwasiliana tena na mchezaji wa Werder Bremen, Milot Rashica, 24, baada ya kumkosa winga huyo raia wa Kosovo msimu uliopita. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO



# TSHABALALA HAENDI YANGA SC - BARBARA

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kuzuka tetesi za beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala' (pichani), ambaye pia anajulikana kwa jina la Zimbwe Jr, kuhamia Yanga, Ofisa Mtendaji Mkuu wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao, Barbara Gonzalez, amewatoa wasiwasi wanachama na mashabiki wa klabu hiyo, akidai kuwa haendi popote na bado ni mchezaji wao halali.

Tangu majuzi zilianza kuzuka tetesi za mchezaji huyo ambaye anaitumikia Simba kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika na kuchaguliwa kwenye kikosi bora cha wiki katika michuano hiyo, lakini hata baadhi ya vyombo vya habari vikiwamo baadahi ya magazeti [si Nipashe] yakiandika kuwapo kwa mpango huo.

**Lakini Barbara amesema kuwa Tshabalala ataendelea kuwa mchezaji wa Simba.**

"Haendi Yanga, ni mchezaji wetu. Ni mchezaji halali wa Simba na Mungu akipenda ataendelea kuwa Simba," alisema Barbara kwa kifupi na msisitizo.

Habari zinaeleza kuwa mchezaji huyo anamaliza mkataba wake kwenye klabu ya Simba mara baada ya msimu huu kumalizika, hivyo klabu ya Yanga inatumia mwanya huo kumshawishi kujiunga na klabu hiyo.

Hata hivyo, tayari klabu ya Simba imedaiwa kumuwekea ofa nono ya kuongeza mkataba wake kwa ajili ya kuendelea kuitumikia klabu hiyo.

Ukiachana na Tshabalala ambaye inaonekana ni ngumu kwa Yanga kumng'oa Simba, lakini habari kutoka ndani ya klabu ya Yanga zinaeleza kuwa inawahitaji pia wachezaji wake wa zamani ambao kwa sasa wako Msimbazi, Gadiel Michael na Ibrahim Ajibu.

Mabingwa wao wa kihistoria inadaiwa kutaka kuwarejesha kundini wachezaji hao ambao wanaonekana hawana nafasi ndani ya Simba kwa ajili ya kukiimarisha kikosi hicho msimu ujao kutokana na kwamba huenda ikashiriki michuano mingi, ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika au Kombe la Shirikisho.

Ajibu na Gadiel ni moja ya wachezaji ambao wanamaliza mikataba yao mwishoni mwa msimu huu na huenda Simba ikaachana nao.

## KVZ nayo yasitisha mazoezi Z'bar

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya KVZ imesimamisha mazoezi yake ya kujiandaa na michezo ya Ligi Kuu Zanzibar hadi utakapomalizika mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

KVZ ni miongoni mwa timu zinazohaha kuusaka ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu ambao utamalizika baada ya mwezi wa Ramadhani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sheha Khamis, alisema kwa sasa wamefunga kuendelea na mazoezi katika kipindi hichi na watarejea mara baada ya kukamilika kwa ibada ya funga.

"Ligi imesimama na sisi tumesimamisha mazoezi, lakini changamoto ipo, hatujui ligi itaendelea lini baada ya Ramadhani ili tupate muda wa kujiandaa, hii ni hatari endapo watasema ligi itaendelea baada ya funga ya sita kwa kuwa timu zitakuwa hazijajiandaa," alisema

Aidha, aliiyomba Bodi ya Ligi Kuu Zanzibar kuangalia uwezekano wa kutoa ratiba ya kumaliza michezo iliyobaki ya ligi hiyo ili timu nazo ziweze kujipanga mapema kwa kujua tarehe rasmi ya kuendelea na ligi hiyo ambayo ipo ukingoni.

KVZ ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na alama 31 sawa na timu ya Mafunzo iliyopo nafasi ya pili katika ligi hiyo inayoshirikisha timu 12 ambapo kwa msimu huu zitashuka mbili.

SH. BILIONI 2...



Mkurugenzi wa Kampuni ya Vunja Bei, Fred Fabian (Kushoto), wakibadilishana mikataba na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, baada ya kutia saini ya mkataba wa kutengeneza na kusambaza jezi pamoja na vifaa vingine vya michezo vya klabu hiyo, jana jijini Dar es Salaam. Mkataba huo wa miaka miwili, unathamani ya Sh. bilioni mbili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Kagera yapania tatu za Simba Kaitaba leo*

Na Shufaa Lyimo

WAKATI leo wakiwakaribisha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Benchi la Ufundi la Kagera Sugar limesema limejipanga vizuri kukutana na Simba katika mchezo wao wa leo watakaoucheza mkoani Kagera, na kuahidi kutoa ushindi wa hali ya juu.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kutoka mkoani Kagera, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Francis Baraza, alisema licha ya kwamba wanakutana na timu kubwa, wamejipanga kuhakikisha wanapata pointi zote tatu wakiwa katika uwanja wa nyumbani wa Kaitaba.

"Tumejipanga vizuri kukutana na Simba katika mchezo wetu wa kesho( leo), nimejipanga kupata pointi tatu nikiwa na lengo la kuiweka mahali pazuri timu yangu, ninaomba mashabiki waendelee kutupa ushirikiano"alisema Baraza.

Kocha huyo alisema mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa kutokana na kila timu ambayo inashiriki Ligi Kuu imejipanga vizuri kupata pointi tatu kwenye kila mchezo ambao inaucheza ili kuhofia kushuka daraja.

"Mchezo utakuwa na ushindani kwa sababu kila timu msimu huu imejipanga kupata matokeo, wachezaji wangu wanaendelea vizuri kila mmoja ana morali ya ushindi kuelekea katika mchezo huo," alisema.

Alisema makosa madogo madogo ambayo aliyabaini kwenye mchezo uliopita ameyafanyia kazi na kudai hayawezi kujitokeza kwa mara nyingine huku akiahidi mashabiki wake kuiweka juu timu hiyo ambayo alikabidhiwa baada ya aliyekuwa Kocha Mkuu, Mecky Maxime kutupiwa virago.

# Michezo

Jumatano Aprili 21, 2021

Nipashe




HABARI UK.22

## Perez: Lazima Haaland, Mbappe watue Madrid

MTAIPENDA TU...




Kocha Mkuu mpya wa Yanga, Mtunisia Nasreddine Nabi, akielezea mikakati yake ndani ya klabu hiyo baada ya kutambulishwa rasmi jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Haji Mfikirwa (Kulia). **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MTUNISIA WA YANGA NA MKAKATI WA KIBINGWA

●●● Ashuka na wasaidizi wawili, ataka muda kuisuka upya huku akieleza anataka kuifanya kuwa...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Klabu Yanga, Mtunisia Nasreddine Nabi, ameeleza mikakati yake mizito ya kuifanyia klabu hiyo baada ya kutua nchini na kuingia mkataba wa mwaka mmoja na nusu, ambapo sasa anachukua rasmi nafasi iliyokuwa imeachwa wazi na Mrundi Cedric Kaze, aliyetimuliwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Nabi alisema anafurahi kuwa sehemu ya benchi la ufundi la Yanga ambayo ni moja kati ya timu kubwa Afrika Mashariki na Kati na anataka kuhakikisha uwezo wake wa kufanya vizuri.

Alisema Yanga ina historia nzuri na ana imani ya kufanya vizuri hapo baadaye kwa sababu ya kulifahamu soka la Afrika.

"Nahitaji muda wa kuandaa timu, kiufundi pamoja na kuweka mipango yangu sawa kwa sababu nimekuja tayari timu iko mwishoni mwa msimu, nina imani kwa ushirikiano mzuri na uongozi tutafikia malengo yanayotarajiwa na Wanayanga," alisema Nabi.

**Kocha huyo aliyewahi kuinoa Klabu ya Al-Merrikh ya Sudan akichukua nafasi ya Mfaransa wa Simba, Didier Gomes, alifutwa kazi ndani ya klabu hiyo baada ya kutopata matokeo mazuri hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.**

Kwa upande wa uongozi wa Yanga, ukizungumza na gazeti hili jijini jana kuhusu ujio wa Nabi, Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Hajji Mfikirwa, alisema kocha huyo amekuja na wasaidizi wake wawili, msaidizi ambaye ni Jawad Sabri na Sghir Hammadi ambaye ni kocha wa viungo.

Alisema wamechukuwa uamuzi huo wa kukubali aje na wasaidizi wake kwa sababu atakuwa na urahisi mkubwa wa kufanya kazi na watu ambao anawafahamu.

"Mpango wa kumleta Nabi kwa sasa ni kuhakikisha kocha huyo anapata muda wa kuona upungufu wa kikosi cha timu yetu kwa ajili ya kufanyia kazi msimu ujao.

"Ujio wa kocha huyo umezingatia pia ushiriki wetu wa michuano ya kimataifa kwa msimu ujao," alisema Mfikirwa.

Alisema kuhusu Kocha Juma Mwambusi, ataendelea kuwapo ndani ya benchi hilo la ufundi akimuelekeza Nabi hadi msimu ujao wataona ni sehemu gani anapaswa kuwapo.

Nabi alipata nafasi ya kuishuhudia timu yake hiyo mpya ikicheza dhidi ya Gwambina FC jana usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Vunjabei aijaza Simba bilioni mbili

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Simba umeonyesha thamani ya ukubwa wake baada ya jana kuingia mkataba wa mabilioni ya shilingi na Mfanyabiashara wa Kitanzania, Fred Ngajiro maarufu kama Fred Vunjabei, kupitia Kampuni yake ya Vunjabei Group kwa ajili ya kutengeneza na kusambaza jezi na vifaa vingine vya michezo.

Mkataba huo ambao ni wa miaka miwili, unathamani ya Sh. bilioni mbili, hivyo kuifanya Simba kuwa klabu ya kwanza Afrika Mashariki na Kati kuingia mkataba mnono kama huo kwa upande wa jezi na vifaa vingine vya michezo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez, alisema Desemba mwaka jana walitangaza tenda hiyo na kujitokeza kampuni 11 binafsi, lakini Fred Vunjabei ndiye aliyeshinda.

Alisema uamuzi wa kumtangaza Vunjabei ni kuwapa fursa wafanyabiashara Watanzania ambao watatoa ajira kwa vijana waliopo mitaani kutangaza bidhaa za Simba kupitia tenda hiyo.

"Tumeingia makubaliano na Vunjabei kwa mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya Sh.bilioni mbili ni tofauti na msimu uliopita ambao awali aliyeshinda tenda hiyo alitoa kiasi cha Sh. Milioni 100," alisema Barbara.

Kwa upande wa Fred Vunjabei, alisema kupitia mkataba huo ana uhakikisha wa kufanya biashara na Simba kwa kuzingatia malengo awali ikiwamo kusambaza bidhaa bora na uhalisia wa hali ya juu yenye nembo ya klabu hiyo.

Alisema mkataba huo umelenga timu zao zote ikiwamo vijana, wanawake na timu kubwa ambayo inawakilisha vema Tanzania kwenye michuano ya kimataifa wakati huu ikiwa imetinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kupitia mkataba huo tutaenda kila mkoa kufungua duka la vifaa vya nembo ya Simba kwa kulipa kodi ya serikali, hivyo tutakuwa makini na kuwachukulia hatua wale wanaouza jezi feki," alisema Fred Vunjabei.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >